SportPesa
TZS. 1,171,243,460
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



Kibaki afariki dunia, ameacha alama ya kudumu

UKURASA 15




Nipashe
Jumamosi Aprili 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580924
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Waziri awatoa hofu wadau mifuko jamii

- Kuhusu taarifa kwamba iko hatarini kufilisika, asema iko imara... *Uk. 2*

## YALIYOMO

### UJENZI WA BWAWA WAWATOKEA PUANI VIGOGO RUWASA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kusimamishwa kazi kwa watumishi wanne wa wizara hiyo kutokana na kusuasua kwa...

UKURASA 3

### UCHUNGUZI MAFUTA YALIYOMWAGIKA UFUKWE BAHARI YA HINDI WAKAMILIKA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema timu iliyoundwa kuchunguza mafuta yaliyoonekana katika ufukwe...

UKURASA 4



Mwonekano tofauti wa majengo ya mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, ambayo ujenzi wake unaonekana kusuasua. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

### Imani potofu, matumizi bangi tishio jipya kwa wavuvi Victoria

UKURASA 3

# CAG abaini tatizo uwekezaji katika mradi wa NHC Kawe

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA PRINCESS, SIMBA QUEENS VITA YA HESHIMA UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mratibu wa masuala ya Virusi vya Ukimwi kitengo cha Polisi Afya, ACP Thomas Kawala, akipata chanjo ya UVIKO-19, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya chanjo hiyo, katika Hospitali ya Polisi, Barabara ya Kilwa, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MAULID MMBAGA.**

# Waziri awaondoa hofu wadau wa mifuko jamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewaondoa hofu wastaafu na watumishi walioko kazini kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii ni himilivu na itaendelea kulipa mafao kama kawaida.

Mifuko hiyo ni wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na ule wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta binafsi.

Kuondolewa kwa hofu kwa wastaafu na wafanyakazi (wastaafu watarajiwa) kunatokana na taarifa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba kuna hatari ya mifuko hiyo kufilisika kutokana na usimamizi usioridhisha.

CAG kwenye ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, alibaini mifuko ya hifadhi ya jamii iko hatarini kupata hasara ya mabilioni ya shilingi kutokana na utekelezaji duni wa miradi yake ya ubia na kampuni mbalimbali.

Akijibu hoja za wabunge zilizojitokeza kwenye mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2022/23, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema mifuko hiyo jamii ni himilivu na itaendelea kulipa mafao kwa wastaafu.

Prof. Ndalichako alisema kati ya mwaka 2018 PSSF ilipoanzishwa hadi Machi 2022, serikali imelipa mafao yenye thamani ya Sh. trilioni 6.91, kila mwezi serikali inalipa Sh. bilioni 58.75 kwa wastaafu 148,868 kila ifikapo tarehe 25 ya mwezi.

"Nikiri kwamba kulikuwa na changamoto hasa kwa wastaafu ambao walikuwa wameanza kazi kabla ya mwaka 1999 ambao walikuwa hawachangii, lakini wakaingia kwenye mfuko kwa hiyo hao walisababisha mfuko uelemewe. Walikuwa hawachangii lakini walitakiwa kulipwa Sh. trilioni 4.62 katika mfuko huo,"alisema.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Ndalichako alisema serikali iliamua kuupa nguvu mfuko kwa kutoa Sh. trilioni 2.17 na kuwezesha kulipa malimbikizo yote ya wastaafu yaliyokuwapo.

"Kutokana na uwezo mkubwa uliotolewa na serikali kwa mfuko wa PSSSF, hivi sasa watumishi wote wanaostaafu wanalipwa mafao yao ndani ya siku 60 baada ya kuleta taarifa zake za kustaafu," alisema Ndalichako.

Hata hivyo, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Bulaya alimpa taarifa Waziri huyo kuwa ripoti ya CAG iliyotolewa hivi karibuni inaonyesha mifuko ina hali mbaya na si himilivu na iko kinyume cha taratibu cha ukwasi wa asilimia 40.

**WALICHOSEMA WABUNGE**

Awali, wakichangia, Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, alisema watumishi kwa sasa wapo kazini lakini hawajui mustakabali wao wakati wa kustaafu.

Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, alisema kwenye jimbo lake kuna watu wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 lakini hawakupewa mafao walipostaafu na kumwomba Waziri Ndalichako awasaidie.

Mbunge wa Sengerema (CCM), Hamis Tabasamu, alisema wastaafu wengi wanapata taabu, wanatembea umbali mrefu kutafuta haki yao.

"Unamwomba mstaafu 'pay slip' ya kwanza aliyoanza kulipwa mshahara miaka 40 iliyopita au barua ya kuthibitishwa kazini, ataipata wapi? Mtaona mvua hazinyeshi kumbe mnafanya dhambi baridi,"alisema.

Mbunge wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave, alisema watumishi wa bandari zaidi ya 100, wanadai maslahi yao kwa muda mrefu hawajalipwa mafao yao na kutaka wapewe fedha zao.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema: "Ucheleweshaji unaofanywa katika kulipa malipo ya wastaafu siyo haki wasiachwe walalamike kwa kuwa walishatoa utumishi wao kwa Taifa na sasa ni zamu ya Taifa kutoa huduma kwao."

# CAG abaini tatizo uwekezaji wa NHC

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAF) amebaini upungufu katika uendelezaji wa mradi wa uwekezaji wa majengo - Kawe mkoani Dar es Salaam.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, CAG Charles Kichere anasema kuwa Aprili 19, 2002, serikali (muuzaji) na kampuni ya Al Ghurair Investment LLC -AGI (mnunuzi) waliingia mkataba wa mauziano ya viwanja namba 697, 709 na 711/1 vyenye ukubwa wa hekari 107.1.

Anabainisha kuwa bei ya mauziano ilikuwa Dola za Marekani milioni 6.5 kwa ajili ya kufanya uwekezaji wa hoteli yenye hadhi ya nyota tano, vituo vya mikutano, maduka, ofisi pamoja na nyumba za hali ya juu.

Hata hivyo, CAG anasema kuwa hadi kufikia mwaka 2012, mnunuzi alikuwa amelipa Dola za Marekani milioni 2.05 tu.

Anaendelea kubainisha kuwa Machi 29, 2012, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) liliingia mkataba wa makubaliano na Kampuni ya Al Ghurair Investment LLC ili kutekeleza ubia wa asilimia 50 kwa 50 kwenye uwekezaji wa Mradi wa Kawe.

CAG anabainisha kuwa NHC ilichukua hatua ya kuunda kampuni maalum ya uendeshaji iitwayo Uptown Kawe Properties Ltd Juni 10, 2014 ili kuendesha mradi huo.

Anasema umiliki wa kampuni maalum ya uendeshaji ulikubalika kuwa sawa kati ya Kampuni ya Al Ghurair Investment LLC na NHC baada ya kutiwa saini kwa makubaliano ya ubia wa kampuni maalum ya uendeshaji.

"Ukaguzi wangu wa maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Kawe ulibaini upungufu ambao unahitaji uangalizi wa serikali. Upungufu huo unajumuisha kutolipwa kwa gharama ya ununuzi wa mali kwa mujibu wa makubaliano yaliyotiwa saini.

"NHC ilitakiwa kulipa Dola za Marekani milioni 3.25 ikiwa ni sehemu yake ya umiliki wa asilimia 50 na Kampuni ya AGI Ghurair Investment LLC ingemalizia kulipa salio la dola za Marekani milioni 1.2, lakini nilibaini kuwa hadi Novemba 2021 pande zote mbili hazikuwa zimelipa fedha hizo," anasema.

CAG anaitaja dosari nyungine kuwa ni kusitishwa kwa uandaaji wa Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Mradi wa Kawe, akifafanua kuwa mnamo Mei 19, 2015, kampuni maalum ya uendeshaji wa mradi (Uptown Kawe Properties Ltd) ilitiliana saini mkataba na Phils International FCZ (mshauri) kwa ajili ya kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa mradi wa Kawe ambao ulitarajiwa kukamilika Novemba 19, 2015.

"Nilibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2021, kampuni mshauri (Phils International FCZ) ilikuwa imekamilisha hatua mbili tu kati ya tano za uendelezaji wa mpango kabambe wa undelezaji wa Mradi wa Kawe," anasema.

CAG anaitaja dosari ya tatu ni mgogoro wa ujenzi katika Kiwanja Namba 711/1 cha mradi wa Kawe, akifafanua kuwa NHC ilichukua hatua binafsi za kuendeleza kiwanja hicho ukihusisha ujenzi wa miradi miwili ya 'Golden Premier Plaza' kwa Sh. bilioni 71 na jengo la 'Seven Eleven' kwa Sh. bilioni 105, yote ikiwa na jumla ya gharama ya Sh. bilioni 176.

"Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa kutokana na matatizo ya kifedha, uendelezaji wa miradi hii ulisitishwa kwa zaidi ya miaka miwili; na hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, kiwango cha kukamilika kwa mradi wa 'Golden Premier Plaza' ulikuwa asilimia 43 na 'Seven Eleven' ulikuwa asilimia 35; na NHC imetumia jumla ya Sh. bilioni 57.98.

"Pia nilibaini kuwa uendelezaji wa kiwanja Na. 711/1 ambacho ni sehemu ya viwanja vya mradi wa Kawe ulitekelezwa bila kumshirikisha na kupewa idhini ya mbia mwenza wa mradi wa Kawe, Kampuni ya Al Ghurair Investment LLC, hali ambayo ilisababisha mgogoro kati ya wabia juu ya suala hilo, na jinsi ya uendeshaji wa kampuni maalum ya uendelezaji wa mradi (Uptown Kawe Properties Ltd).

"Pia nilibaini uendelezaji wa kiwanja namba 711/1 ulifanywa kabla ya kukamilika kwa mpango kabambe wa undelezaji wa mradi wa Kawe.

"Nina maoni kuwa ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi wa Kawe ulishikilia mtaji wa NHC ambao ungewekezwa kwenye miradi mingine yenye faida.

"Pia ucheleweshaji unaongeza gharama za mradi kwa kuendelea kuongezeka kwa gharama za vifaa na adhabu zingine zinazohusiana na uchelewaji wa uendelezaji," anatahadharisha.

CAG ana angalizo kwamba kazi za ujenzi katika kiwanja namba 711/1 zinaweza kusababisha mgogoro wa kisheria dhidi ya NHC; mgogoro huo unaweza kuathiri hatma ya umiliki wa NHC kwenye mradi wa Kawe.

"Ninapendekeza NHC iihusishe serikali ili kutafuta namna bora ya kutatua masuala ambayo yanachelewesha kukamilika kwa mradi wa Kawe," CAG anawasilisha hoja yake.

## HABARI KITAIFA

# Ujenzi wa bwawa wawatokea puani vigogo wanne RUWASA

**Na Romana Mallya**



WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso (pichani), ameagiza kusimamishwa kazi kwa watumishi wanne wa wizara hiyo kutokana na kusuasua kwa ujenzi wa bwawa la Kwankambala, linalojengwa Handeni mkoani Tanga.

Walioagizwa kusimamishwa ni watumishi na viongozi kutoka Wakala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Makao Makuu akiwamo msimamizi wa mradi, Hamisi Matungulu.

Wengine ni Mhasibu Mkuu, CPA Jimmy Mwanyakunga, Meneja Udhibiti Ubora wa Miradi na Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi, Amos Mtweve na Mkurugenzi wa Ununuzi na Ugavi, Zam Mlimira.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali wa wizara hiyo, lorence Temba, ilisema Waziri Aweso ametoa agizo hilo jijini Dodoma akiwa kwenye kikao na wadau wa sekta ya maji wa Handeni.

Taarifa hiyo ilisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya ziara ya kikazi aliyofanya Waziri Aweso Aprili 12, mwaka huu, wilayani humo na kubaini mkandarasi anayejenga bwawa hilo amelipwa Sh. milioni 602.8 sawa na asilimia 33 ya gharama ya mkataba na kazi iliyofanyika ni asilimia 20 zilizopangwa kufanyika.

Pia ilisema iligundulika kampuni iliyopewa kazi hiyo, iitwayo Civil Loth Enterprises Ltd iliondoa vifaa vya kazi katika eneo la ujenzi, wakati iliongezewa muda wa utekelezaji wa ujenzi huo.

Taarifa hiyo ilisema kikao hicho kilichoongozwa na Waziri huyo kimetaka kufanyika mapitio ya mkataba wa nyongeza wa mkandarasi.

Pia kimetaka Katibu Mkuu, Wizara ya Maji kuunda tume ya uchunguzi ili kubaini matatizo yanayokabili utekelezaji wa mradi na kushikiliwa kwa Mkandarasi Civil Loth Enterprises Ltd kwa hatua za uchunguzi zaidi.

Ilisema hatua nyingine za kukwamua ujenzi wa bwawa hilo zinaendelea.

# Imani potofu, matumizi ya bangi tishio jipya wavuvi Ziwa Victoria

**Na Daniel Limbe,** CHATO

IMANI potofu ya matumizi ya bangi kwa wavuvi katika Ziwa Victoria imetajwa kuwa tishio jipya kwa vijana na watoto.

Vijana hao huamini kuwa wanapotumia dawa ya kulevya aina ya bangi, hupata samaki wengi sambamba na ongezeko la nguvu za kufanya kazi nyakati za usiku.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kwamba matumizi ya bangi kwenye mialo ya wavuvi wa samaki unatokana na kutokuwepo kwa udhibiti kutoka mamlaka husika.

Aidha, upatikanaji wa dawa hizo umekuwa mwepesi zaidi kwa siku za karibuni kutokana na wauzaji na wasambazaji kubuni njia ya kupitisha ziwani, ikilinganishwa na awali walipokuwa wakipitisha kwa njia ya barabara.

Habari kutoka chanzo cha habari (jina linahifadhiwa) kimeieleza Nipashe kuwa dawa hizo zinazalishwa kwa wingi kwenye visiwa ndani ya Ziwa Victoria, huku watumiaji wengi wakiwa vijana na baadhi ya watoto wanaojihusisha na shughuli za uvuvi.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya Ziwa Victoria (BMU) mwalo wa ufukwe wa Chato, Kamese Malima, anakiri kuwapo kwa matumizi ya bangi kwa baadhi ya wavuvi wanaotumia mwalo huo.

"Ni kweli wako wavuvi wanaotumia bangi kabla na baada ya kwenda kuvua samaki. Japo mimi si msemaji katika suala hilo, ninavyoona udhibiti wake unakuwa mgumu kutokana na baadhi ya viongozi kufumbia macho," alisema Kamese.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chato, Makonzere Phinias, alithibitisha matumizi ya bangi kwa wavuvi walioko kwenye kijiji chake, huku akisema amekuwa akichukua hatua za kuwaelimisha kuachana na matumizi holela ya dawa hizo.

**KAULI YA DCEA**

Kwa mujibu wa Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), Dk. Peter Mfisi, bangi haina uhusiano wowote na imani za kufanikiwa kupata samaki kwa wingi ndani ya maji.

"Bangi inavutwa mwilini wakati samaki wako ndani ya maji na mvutaji akimaliza kuweka nyavu zake huondoka na kurejea baadaye. Kungekuwa angalau na ukweli kiasi iwapo bangi ingelikuwa inatandazwa na nyavu halafu samaki wakapatikana lakini kinachofanyika ni kuvutwa na kubaki mwilini,"anasema.

Dk. Mfisi anasema ni ukweli kuwa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nao wamejiingiza kwenye matumizi ya bangi, huku akisema ni kichocheo kikubwa cha vijana kujidunga sindano wakiamini wanapunguza mawazo na baadhi yao kuwa na imani potofu za kuongeza akili za kufikiri.

Mbali na bangi, dawa zingine zinazotumika nchini ni pamoja na heroin, mirungi, cocaine, petroli pamoja na gundi.


## NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | MADALE KIDS PALACE | NYUMBA YA BIASHARA | CRUCIAL INVESTMENT LIMITED | MADALE | 10/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JOYCE STEVEN MSOFU | NYUMBA | MONICA THADAYO CHISUMUNI | NG'HONG'HONA | 10/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | HAPPYNESS MUSSA JEGU | NYUMBA | HAPPYNESS MUSSA JEGU | NZUGUNI A-DODOMA | 11/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | BIMLA ELECTRICAL SUPPLIES | VIWANJA VIWILI | RAJABU SIMEO MAJIGE | BUIGIRI- CHAMWINO | 11/05/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | EUGEN RAYMOND MGAYA | GARI TOYOYA IST T343 DCS | EUGEN RAYMOND MGAYA | DODOMA MJINI | 12/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | HILDA DEOGRATIUS MKAWE | NYUMBA | DEOGRATIAS IGNAS MKAWE | DARAJA MBILI-ARUSHA | 10/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MAGDALENA KISACK KWAYU | NYUMBA | MAGDALENA KISACK KWAYU | LEMARA-ARUSHA | 12/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | SASI SELEMANI KITUNDU | NYUMBA | MWAJUMA SELEMANI KITUNDU | GOBA KUNGURU | 11/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MUSBATI HASSAN KIBERITI | NYUMBA | ANSET JOSEPH MJUMARE | MANZESE | 10/05/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | NYUMBA | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | KIMARA STOP OVER | 12/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | ALEX NAHUMU PALANGYO | NYUMBA | JOSEPH BENJAMINI | MBEZI MTONI | 11/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | FREDY SAMSON LILENGA | NYUMBA | FREDY SAMSON LILENGA | MAKONGO KASKAZINI | 12/05/2022 NA KUENDELEA |
| TANDALE | REMY SALEWI IWASHA | NYUMBA | RAJABU SALEHE KHALFAN | MBAGALA | 13/05/2022 NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JUMA SEIF MUSSA | NYUMBA | JUMA SEIF MUSSA | KICHANGANI | 17/05/2022 NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JENEROSE ANNA LUZWILO | NYUMBA | JANE ANNA LUZWILO | BUZA | 18/05/2022 NA KUENDELEA |
| TEMEKE | YASINI MBAGO MOHAMED | NYUMBA | YASSINI MOHAMED MBAGA | BANGULO-PUGU STATION | 19/05/2022 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0785242219/0754497396/0714939933
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Uchunguzi mafuta yaliyomwagika ufukwe Bahari ya Hindi wakamilika

**Na Romana Mallya**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema timu iliyoundwa kuchunguza mafuta yaliyoonekana katika ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la feri jijini Dar es Salaam, imekamilisha kazi.

Kutokana na kukamilika kwa uchunguzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, amesema jana kuwa kwa sasa timu hiyo inaandaa ripoti itakayowasilishwa muda wowote kuanzia sasa.

Akizungumza na Nipashe juzi kuhusiana na uchunguzi ilioutangaza kuufanya, Dk. Gwamaka alisema: ""Timu bado inaendelea kuandaa ripoti imeshafanya ukaguzi. Suala linakuwa gumu kwa sababu pale kuna mabomba yako zaidi ya 12, kujua ni lipi linalovuja kunahitajika utaalam na kuthibitisha ndicho kinachofanyika. Bado timu haijatoa ripoti yake."

Aprili 7, mwaka huu, taharuki ilizuka baada ya taarifa kutolewa kuwa meli isiyofahamika imemwaga mafuta ambayo wananchi waliyasomba kwenye madumu.

Baada ya tukio hilo, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, Canute Msacky, alisema baada ya kupata taarifa za tukio hilo waliwakamata watu sita pamoja na madumu ya ujazo wa lita 20 na mengine madogo sita yakiwa yamejazwa mafuta hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngw'ilabuzu Ludigija, alifika eneo hilo na kuwatahadharisha wananchi wa Dar es Salaam na maeneo mengine ya Pwani kuwa makini na ununuzi wa mafuta yaliyowekwa kwenye madumu, huku akielekeza mamlaka husika zichunguze athari za mafuta hayo.

Baada ya kuwapo kwa taarifa hizo, Dk.Gwamaka alisema NEMC ilitarajia kuanza uchunguzi wa tukio hilo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na wanaoingiza mafuta ili kubaini aliyefanya uchafuzi huo wa mazingira.

Alisema walijaribu kuzungumza na baadhi ya waliowahisi lakini walikataa kufanya uchafuzi huo.

"Hapo nyuma tuliwahi kupiga faini kampuni kadhaa lakini bado hali hii inajitokeza. Tumewataka wenye mabomba ya mafuta wayakarabati au kuweka mapya, tutakapompata aliyefanya uchafuzi huu atapewa adhabu kubwa," alisema.

Alibainisha kuwa mafuta yanapomwagwa kwenye bahari husababisha athari kwa viumbe hai, mikoko pamoja na wadudu kufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni.




Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (wa pili kulia), akikabidhi viti na meza kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mwanalugali ya mkoani Pwani, Joseph Mkumbo, wakati wa mahafali ya kwanza ya kidato cha sita, shuleni hapo juzi. Kulia ni Meneja wa NMB Tawi la Kibaha, Festo Issango na (katikati) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Joyce Mori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG amulika athari UVIKO-19 kiuchumi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amefanya ukaguzi kuhusu athari za uchumi katika Sekta ya Utalii kutokana na janga la UVIKO-19.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Fedha na Mipango, Sekta ya Utalii inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa huku ikiingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa wiki iliyopita, CAG Charles Kichere anasema nchi zote duniani zimechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na janga la UVIKO-19.

Anasema hatua hizo ni pamoja na kuweka vizuizi vya usafiri, karantini, amri za kutotoka nje, kufunga mipaka au vizuizi kwa abiria wanaoingia kwenye nchi husika, ulazima wa kupima UVIKO-19 kwenye viwanja vya ndege na maeneo mengine ya kungilia nchini na ushauri kwa usafiri kuhusu maeneo yenye kasi ya maambukizi ya UVIKO-19.

CAG Kichere anasema vitendo hivyo vimeathiri kwa kiwango kikubwa mienendo ya watu kusafiri sehemu mbalimbali duniani, ikiwamo Tanzania.

Anabainisha kuwa katika mwaka 2020/21, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) lilipokea watalii 511,801 na kukusanya mapato ya Sh. bilioni 56.98 wakati kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20 ilipokea watalii milioni 1.08 na kukusanya mapato ya Sh. bilioni 250.97.

Anasema hali hiyo inaonyesha kupungua kwa mapato kwa Sh. bilioni 193.99 (sawa na asilimia 77) na watalii 565,589 (sawa na asilimia 52) kulinganishwa na mwaka uliopita.

Kwa upande mwingine, CAG anasema Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) katika kipindi hicho ilikusanya Sh. bilion 31.42 kutokana na watalii 191,614 huku mwaka 2019/20 kikusanya Sh. bilioni 143.52 kutokana na watalii 609,984.

Hali hiyo inaonyesha kupungua kwa mapato kwa kiasi cha Sh. bilion 112.1 (sawa na asilimia 78) na watalii 418,370 (sawa na asilimia 69) kulinganishwa na mwaka uliopita.

"Moja ya athari kubwa za janga la UVIKO-19 ni kupungua kwa idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi za taifa na kuathiri Sekta ya Utalii.

"Ninapendekeza serikali ichukue hatua za kuhakikisha huduma za kiafya na usalama zinapewa kipaumbele kwenye hifadhi za taifa ili kuongeza imani ya watalii.

"Hatua hizi zijumuishe uwapo wa vifaa vya kutosha vya usafi na vituo vya muda kwa ajili ya kutenga watu watakaogundulika kuwa na dalili za UVIKO-19," CAG anawasilisha hoja yake.

**UTALII WA FARU**

CAG pia anabainisha kuwa amebaini kuchelewa kuanzishwa kwa eneo maalum kwa ajili ya utalii wa faru ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Anafafanua kuwa serikali kupitia Hifadhi ya Taifa Serengeti ilipanga kutambulisha eneo maalum la utalii wa faru ambalo lilitarajiwa kufunguliwa Agosti 2021.

"Hifadhi ya Serengeti ina maeneo matatu maalum kwa ajili ya faru ambayo ni Moru, Nyamalumbwa na Ndasiata. Maeneo haya yana vivutio vingine vya utalii kama vile Ziwa Magadi, 'Jiwe la Msumi' na mapambo ya jamii ya Wamasai.

"Ukaguzi wangu ulibaini kuwapo miongozo ya utalii wa faru na ada iliyopangwa kwa ajili ya utalii wa faru. Hata hivyo, hadi ninakamilisha ukaguzi wangu mwezi Novemba 2021, eneo hilo maalum la utalii wa faru halikuanza kutumika kutokana na changamoto kadhaa.

"Baadhi ya changamoto hizo zilizohitaji kutatuliwa kwanza ni pamoja na: Kuhamishwa kwa Hoteli ya Sopa, Kambi ya Kusini na Magadi ambavyo vipo katika eneo hilo; uboreshaji wa barabara; kutengeneza eneo la pikniki; na kuimarishwa kwa usalama wa faru.

"Kwa maoni yangu, kuchelewa kuanza kufanya kazi eneo maalum la utalii wa faru kunainyima Hifadhi ya Serengeti mapato kwani watalii wangekuwa wanavutiwa na utalii huo, hivyo kuongezeka na kukuza mapato ya hifadhi.

"Ninapendekeza serikali kupitia TANAPA, ishughulikie changamoto zote zilizoainishwa zinazosababisha utekelezaji wa mradi huu kusimama," CAG anawasilisha hoja

# Watendaji kata nchini kumwagiwa pikipiki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema katika mwaka wa fedha ujao wa 2023/24, serikali itawanunulia pikipiki watendaji wa kata nchini ili kurahisisha utendaji kazi wao.

Bashungwa alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu hoja za wabunge zilizoibuliwa kwenye mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2022/23.

Alisema serikali inatambua kazi wanayofanya na katika bajeti ijayo watapatiwa usafiri kama ilivyofanyika kwa Maofisa Ugani.

Pia aliwaagiza wakurugenzi kuzingatia matakwa ya sheria ya kutoa posho ya Sh.100,000 kwa watendaji wa kata kila mwezi.

"Kwenye baadhi ya halmashauri, watendaji wa kata wamekuwa wakifuatilia kana kwamba hii ni hisani. Niwaelekeze wakurugenzi wahakikishe wanapata hii hela kila mwezi kwenye kata yake hii si hisani," alisema.

Aidha, alisema mfumo wa maombi ya ajira kuna tatizo la mtandao lakini timu yake inafanya kazi kuhakikisha wanaoomba wanafanikiwa kukamilisha maombi yao kwa njia ya mtandao.

Kuhusu machinga, alisema Rais ameagiza kuwekwa mazingira rafiki kwao na kuwapanga kwa utaratibu ambao msuli hautumiki wala kuchukua mali zao.

"Wakuu wa mikoa wanaelekezwa kuwa machinga, bodaboda na mama lishe ni maeneo yana hisia tutoe taarifa TAMISEMI. Kama kutakuwa na operesheni yoyote ili serikali ifuatilie kwa kina kile kinachofanyika kwa wamachinga," alisema.

Bashungwa alisema dhamira ya serikali ni kuweka mazingira rafiki kwao na kuwa na matumaini kwa wanayoitegemea sekta ya machinga. Kuhusu ujenzi wa nyumba za walimu, alisema kila mwaka wa fedha serikali itakuwa ikitenga fedha kwa ajili ya nyumba za watumishi.

"Tumekubaliana baada ya kupitishwa bajeti hii tukutane Wizara mbili ya TAMISEMI na Utumishi tujipange kwa mambo mliyoelekeza na bajeti zetu,"alisema.

# Wanasheria wafundwa kuhusu utendaji kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka wanasheria wake kutekeleza majukumu yao kwa bidii,weledi, na uadilifu wa kiwango cha juu kwa maslahi mapana ya taifa ili kuisaidia kupata ushindi kwenye mashauri mengi na kupunguza migogoro na wadau wake.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Dk. Ndumaro alisema badala ya kuendelea kufanya kazi kwa mazoea, wanasheria wa serikali wanapaswa kubadilika katika utendaji wao wa kazi wa kila siku.

"Natoa rai kwenu mwendelee kutekeleza majukumu yenu kwa bidii, weledi na uadilifu wa kiwango cha juu kama mnavyotarajiwa kwa maslahi mapana ya taifa. Kwa kufanya hivyo mtaiwezesha serikali kupata ushindi kwenye mashauri mengi na kupunguza migogoro baina ya serikali na wadau wake," alisema.

Aidha, aliwata kuendeleza juhudi za serikali katika kupambana na kuziba mianya yote ya rushwa.

"Aidha majadiliano na upekuzi wa mikataba mbalimbali vyote vilenge kuongeza tija na kulinda maslahi mapana ya nchi yetu." alisema

Pia alisisitiza wanasheria kufahamu vipaumbele vya serikali na jinsi watakavyo vitekeleza katika mipango yao.

"Kila mtumishi anapaswa kushiriki katika sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti kwa kujiandikisha na kuhesabiwa. Kila mtumishi awe mbunifu na kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufikia malengo ya ofisi na taifa kwa ujumla," alisema.

Dk. Ndumbaro pia aliwataka watumishi kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya utumishi ili kuongeza tija na ubora wa kazi na kuongeza imani kwa wadau wao.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema lengo la mkutano huo wa Baraza la wafanyakazi ni kupokea na kujadili taarifa ya mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

"Kama mnavyofahamu ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipeleka serikalini maombi ya kuongezewa fedha katika bajeti yake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuishauri serikali katika masuala yote ya kisheria," alisema.

Alisema maeneo ambayo yamepewa kipaumbele kwenye bajeti ya 2022/2023 ni kufanya urekebisho wa sheria ili kutoa toleo la sheria la mwaka 2022.

Pia alisema mpango mwingine ni kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji huduma za kisheria, kuendesha mashauri ya madai na jinai mahakamani.




Baadhi ya washiriki wa semina za kila Jumatano zinazoendeshwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wakiwa kwenye mjadala kuhusu huduma ya bure kwa mwanamke mjamzito, katika makao makuu ya mtandao huo, Mabibo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC awa mbogo upigaji mabilioni mikopo ya watu wenye ulemavu

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameshtukia 'upigaji' wa Sh. bilioni tano zilizotengwa kwa ajili ya kukopesha vikundi vya walemavu, vijana na wanawake mkoani hapa.

Kutokana na hatua hiyo, Gabriel ameagiza kusimamisha mishahara ya watumishi wa halmashauri zilizohusika na upotevu wa fedha hizo.

Akizungumza jana katika kikao kazi kilichowakutanisha watumishi wa sekta ya afya na elimu, Gabriel alisema, 'upigaji' huo umefanywa bila Baraza la Madiwani kujua.

Gabriel pia aliagiza watumishi wote waliohusika waliopo mkoani Mwanza wakiwamo na wale waliohamishiwa mikoa mingine, wachukuliwe hatua.

"Fedha nyingi hizi zimeibwa yaani hakuna hata tangazo, mchakato wowote wa kuidhinisha fedha hizo na mbaya zaidi baraza la madiwani halijui," alisema.

Alibainisha kuwa uchunguzi uliofanywa umebaini kulikuwa na vikundi hewa na walipofuatilia zaidi walibaini pia hapakuwa na majina ya vikundi bali ya watu binafsi. Aidha, alibainisha kwamba imebainika kuwapo ununuzi wa magari yaliyotumika kwa gharama kubwa ikiwa ni ukiukwaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake.

Hata hivyo, mkuu huyo wa mkoa hakusema ni halmashauri gani iliyohusika na sakata hilo, lakini alisema waliofanya wizi huo ni watumishi wa serikali mkoani kwake.

Wakati hayo yalitokea mkoani Mwanza, tayari ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/2021 imebaini 'madudu' ya wizi katika sekta mbalimbali zikiwamo halmashauri.

Katika hatua nyingine, Gabriel alikabidhi zawadi ya kombe kwa wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kama motisha kwa kuibuka vinara katika utekelezaji wa miradi ya serikali kwa wakati.

Akitoa zawadi hiyo, Gabriel alisema kuwa wilaya ya Ilemela imekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya serikali.

Katibu Tawala mkoani Mwanza, Ngusa Samike, aliwataka madiwani na mameya kuacha tabia za kuhoji kila maelekezo ya utekelezaji wa miradi ili kuepusha ucheleweshwaji wa miradi.

"Kupitia zawadi hii tujimejifunza kitu kwa Wilaya ya Ilemela, niwatake sasa Madiwani na Mameya kuacha tabia ya kuhoji kila maelekezo mnayoyapokea kwani siyo kila maelekezo yanatokea mkoani mengine ni ya kitaifa, tuyafanyie utekelezaji haraka kuepusha kukwamisha shughuli za kimaendeleo," alisema.

# Mwongozo sensa ya majengo waandaliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa Mwongozo wa uhamasishaji utakaohakikisha kila jengo nchini linahesabiwa katika sensa ya majengo inayotarajiwa kufanyika Agosti, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akifungua kikao kazi cha wadau kuhusu maandalizi ya sensa ya majengo.

Alisema mwongozo huo utawahusisha wananchi wote, wamiliki wa majengo wote nchini, serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, taasisi na mashirika ya umma, taasisi za kidini, vyama vya ushirika, vyama vya siasa na wadau wengine kama vile wapangaji, walinzi wa majengo na ndugu wa wamiliki majengo.

"Aidha, mwogozo pia utaeleza wajibu wa kila mmoja niliyemtaja hapo juu nitoe rai kwa kila mwananchi kuhakikisha nyumba na majengo yao yanahesabiwa," alisema Kikwete.

Ridhiwani alitoa pongezi kwa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake kufanya sensa ya majengo sambamba na sensa ya watu na makazi kwa mwaka 2022.

"Aidha naendelea kuwapongeza wataalamu wote wanaoshiriki maandalizi ya sensa kwa kazi nzuri wanazofanya. Nitoe rai wananchi wote kutoa ushirikiano mkubwa kwa wataalamu watakaoshiriki sensa ya majengo ya mwaka 2022 ili kuhakikisha kwamba azma ya serikali ya upatikanaji wa taarifa za majengo zilizo sahihi inafikiwa kwa manufaa ya umma," alisema.

Alisisitiza kuwa endapo mmiliki au mwakilishi wake kwa sababu yeyote hatakuwepo wakati wa sensa basi anaagiza kujaza fomu maalumu itakayokuwepo katika ofisi ya serikali ya mtaa, kijiji au kitongoji na kuikabidhi kwa mtendaji au mwenyekiti wa serikali za mitaa.

"Na hii ni pamoja na wale wanaomiliki misingi ya nyumba, nyumba ambazo ujenzi wake unaendelea na maboma," alisisitiza.

Pia alisema kutokana na umuhimu wa sensa hii serikali inaendelea na maandalizi ya kufanikisha zoezi hilo kwa kutenga fedha, rasilimali watu, na vifaa ili kufanikisha sensa ya kwanza ya majengo nchini.

"Madhumuni makuu ya kufanya sensa ya majengo ni kukusanya taarifa za majengo yote nchini ili kupata takwimu za majengo, kupima hali ya umaskini usio wa kipato kwa wananchi ili kuwezesha kutathimini na kupanga maendeleo ya miji na wakazi wake," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, aliwataka wadau hao kutumia kikao hicho kutoa maoni yatayowezesha kufanikisha sensa ya majengo.

"Hili ni zoezi linafanyika kwa mara ya kwanza nchini hivyo inawezekana tukapatia au tukakosea hivyo mjitahidi kufanya kwa umakini kwani aibu itakayotokea si ya serikali tu hata nyie mnahusika tufanye kitu ambacho pia mataifa mengine watakuja kujifunza," alisema Dk. Kijazi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Masikio, macho, akili zote zaitazama Simba

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania na Afrika Mashariki waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba kesho watashuka ugenini Afrika Kusini kuwavaa wenyeji, Orlando Pirates.

Ni katika mechi ya mkondo wa pili wa mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kupata ushindi wa bao 1-0, katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Simba au Wekundu wa Msimbazi kama inavyoitwa na mashabiki wake inahitaji sare au ushindi wa aina yoyote ili kupata tiketi ya kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatakiwa kushuka uwanjani katika mchezo huo kwa nidhamu na kuwaheshimu wapinzani wao kutokana na ubora ambao wanao wanapokuwa nyumbani, lakini pia wakiwa na faida ya kucheza mbele ya mashabiki wao.

Simba inatakiwa kuingia uwanjani ikifahamu inapeperusha bendera ya Tanzania na kwa wao kufanya vyema, si tu kutaibeba jina la klabu yao, lakini kutalipa taifa heshima ambayo imeikosa kwa muda mrefu kupitia michuano hiyo, maana ni muda umepita hakuna timu ya hapa nchini iliyofika hatua ya nusu fainali.

Wachezaji wa Simba wanatakiwa kuingia uwanjani wakisahau bao moja ambalo walipata hapa nyumbani ili kujiweka kwenye mazingira ya kuendelea kupambana na kujipanga kusaka ushindi.

Kama wachezaji wa Simba wataendelea kujituma na kucheza katika kiwango bora kama walivyofanya kwenye mechi zilizopita walipocheza nyumbani, hakika watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi na hatimaye kutimiza ndoto na malengo waliyojiwekea ya kucheza nusu fainali au fainali ya michuano hiyo.

Nipashe tunawakumbusha Simba hakuna kisichowezekana, kama iliwahi kuwavua ubingwa wa Afrika vigogo wa Misri, Zamalek tena wakiwa nyumbani kwao, kesho pia inawezekana kwa wao kupata matokeo chanya na hatimaye kusonga mbele.

Huu ni wakati wa Watanzania kuweka pembeni tofauti za kishabiki na kilichobakia ni kuiombea Simba dua njema kwa sababu mafanikio yake pia yataibeba Afrika Mashariki, ambayo kwa muda mrefu timu zake zimekuwa zikitolewa mapema kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Mbali na Simba kuvuna kitita kikubwa cha fedha endapo itasonga mbele, lakini itaihakikishia Tanzania Bara kupata wawakilishi wanne katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika katika msimu ujao, lakini pia Zanzibar ikitoa timu nyingine mbili.

Kimsingi ni jambo gumu kwa wapinzani wao hasa Yanga kuwaombea dua njema, lakini moyoni wanafahamu matunda ambayo Tanzania itayapata endapo Simba itasonga mbele katika michuano hiyo, hivyo ni muda sahihi kwao kuunganisha nguvu kuwaombea watani zao mafanikio.


Katika kuhakikisha Simba inafanya vyema, huu ni wakati mwingine kwa viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kukaa karibu na wawakilishi hao ili kuhakikisha maandalizi yao ya kuwavaa Orlando Pirates yanamalizika bila ya kuwapo kwa vitendo vyovyote vya hujuma na hatimaye kiu ya kutinga hatua ya nusu fainali inatimia.

Tunafahamu katika mchezo wa soka au mingine yoyote, miujiza ni jambo lisilotarajiwa, lakini huu ni wakati wa kuiombea Simba iwe yenye bahati nzuri kwa siku ya kesho.

Kila mwanamichezo, kwa nafasi yake na imani yake, huu ni wakati wa kuwaombea dua njema Wekundu wa Msimbazi na kuweka pembeni utani wa jadi na upinzani wa ligi ya hapa nyumbani.

Kila la kheri Simba SC, kila la kheri Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tukijipanga, kwenda AFCON inawezekana

Na Adam Fungamwango

**NI** wiki ambayo Watanzania walishuhudia Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ikipangwa kwenye Kundi F kuelekea kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Ivory Coast.

Shirikisho la Soka Afrika (CAF) lilichezesha droo ya michuano hiyo na Tanzania ikaangukia kwenye kundi ambalo lina timu za Algeria, Uganda na Niger.

Mara tu baada ya droo hiyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen alisema kundi hilo ni moja kati ya makundi magumu, lakini akasema wako tayari kwa michuano hiyo, kikubwa tu akasisitiza uwajibikaji wa pamoja na maandalizi mazuri. " Algeria ni timu kubwa, Uganda ni timu nzuri ambayo wametuzidi kwenye viwango vya soka, Niger sijui sana habari zao, lakini mechi zitakuwa ngumu, kila mtu sasa ana wajibu kuanzia viongozi, benchi la ufundi na wachezaji ili tufuzu AFCON, kifupi tuko tayari kwa mashindano. Nadhani maandalizi ndiyo kitu kikubwa, tutacheza mechi mbalimbali za kirafiki ili kujiweka sawa," alisema kocha huyo na akaongeza:

"Tofauti ya michuano hii ni kwamba zinafuzu timu mbili za juu kwa hiyo ni faida kwetu, hii ni tofauti ya ile ya kufuzu Kombe la Dunia ambapo timu moja tu ndiyo ilikuwa inasonga mbele," alisema Poulsen.

Si yeye tu, hata makocha wengine walitoa maoni yao mbalimbali na nini cha kufanya ili kuiwezesha Tanzania kufuzu fainali hizo. Mmoja wapo alikuwa na Juma Mwambusi ambaye alikiri ni kundi gumu na kutahadharisha tusidharau wala kubweteka.

"Hakuna timu rahisi, zamani ikiandikwa Niger tunasema haina kiwango, lakini kwa sasa wako vizuri kimiundombinu ya soka na wana wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi yao tofauti na sisi, kwa hiyo ni kundi gumu. Inahitajika jitihada kubwa kuhakikisha tunaweza kufanya lolote, mimi naamini kwa vijana wetu kama wakiweza kujitambua tunaweza kupita," akasema kocha huyo na kusisitiza.

"Tukiwatumia wachezaji wanaocheza nje ya nchi ambao nimewaona kwenye mechi zilizopita, wanaweza kutusaidia, ligi yetu kwa sasa ina ushindani, lakini tunahitaji mechi za majaribio nyingi, na tucheze na timu za Afrika Kaskazini na mataifa walioendelea kisoka na pia tupate mechi ambazo tukachezee ugenini, siyo kila mechi ya kirafiki tunacheza hapa hapa, hatutusaidia," akasema.

Yote yaliyosemwa hapa yana mchango mkubwa kufanikisha amza ya Tanzania kufuzu fainali hizo kwa mara ya tatu tangu ipate Uhuru. Mwanzo ilikuwa mwaka 1979, na fainali zake zikachezwa 1980 nchini Nigeria, na mara ya pili ni 2019 huko Misri.

Tunatarajia maandalizi yataanza mapema, na kila mmoja awajibike kwenye nafasi yake kama alivyosema Poulsen, na Mwambusi amesisitiza kutoidharau timu yoyote, pia mechi ya kirafiki kwa sasa zikachezwe nje ya nchi. Ni kweli kabisa, kwa miaka ya karibuni hatujaona Stars ikienda kucheza mechi za kirafiki zilizo kwenye kalenda ya FIFA nje ya nchi.

Watanzania sasa tuanze kufanya juhudi za kuwasisha wachezaji Stars kuutumia vyema uwanja wa nyumbani kwa sababu ndiyo moja kati ya vitu vinavyowafelisha.

Stars inaweza kushinda au kutoa sare ugenini, lakini ikafungwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Kama tunataka kwenda Ivory Coast tusikubaliane na hilo.

Halafu maandalizi ya kisayansi yapewe zaidi nafasi kuliko kuundwa kamati za hamasa nyingi ambazo hazijulikani zinafanya kazi gani, badala yake zinaleta mkanganyiko tu usio na maana.

Kikubwa baada ya maandalizi mazuri, kutumia mechi tatu za nyumbani vizuri na kuisaka japo pointi moja ya ugenini kwa timu yoyote ile kati ya hizo. Nina uhakika tunaweza kufuzu AFCON.

# Sababu kupanda kwa mbolea zatajwa

BUNGE limeelezwa kuwa katika msimu wa 2021/22 bei za mbolea zimeendelea kupanda kwenye soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19 na Vita vya Russia na Ukraine.

Athari hizo zinatajwa kusababisha kupungua kwa uzalishaji na ongezeko la gharama za malighafi zinazotumika kutengeneza mbolea. Kutokana na hali hiyo, serikali imeanza kuchukua hatua za haraka, muda wa kati na muda mrefu katika kukabiliana na tatizo hilo la kupanda kwa bei.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza.

Katika swali lake, Njeza alihoji serikali ina mkakati gani wa kupunguza bei za mbolea zinazopanda kwa kasi kubwa kwenye soko la dunia ili kumpunguzia mkulima mzigo.

Mavunde, akijibu swali hilo, alisema hatua za haraka ni pamoja na kudhibiti upandaji holela wa bei usiozingatia gharama halisi za uingizaji wa mbolea nchini kwa kutangaza bei elekezi zinazopaswa kuzingatiwa na wafanyabiashara katika maeneo ya uzalishaji.

"Serikali imekutana na uongozi wa kiwanda cha mbolea cha Minjingu kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto za kiwanda ili kuhakikisha kinaongeza uzalishaji wa mbolea kutoka wastani wa tani 30,000 hadi kufikia tani 100,000 kwa mwaka," alisema.

Pia alisema serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji wapya wa viwanda vya mbolea ambapo kampuni ya Itracom Fertilizers Limited kutoka Burundi imejitokeza na inajenga kiwanda katika mkoa wa Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka.

"Hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zitasaidia kupunguza bei ya mbolea," alisema Mavunde.

## Wizara yakamilisha Ujenzi majosho 168

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imekamilisha ujenzi wa majosho 168 katika halmashauri 80 kwa gharama ya Sh. bilioni 3.033.


Waziri wa Wizara hiyo, Mashimba Ndaki, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu.

Katika swali lake, Kingu alitaka kujua lini Serikali itajenga majosho ya kutibu mifugo katika kata za Makilawa, Igelansoni, Iyumbu, Ighombwe, Mgungira na Mwaru wilayani Ikungi ili kuwasaidia wafugaji.

Akijibu swali hilo, Ndaki alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, wizara inakamilisha ujenzi wa majosho hayo.

Aidha, alisema kati ya majosho hayo, majosho mawili yanajengwa katika kata za Mgungira na Siuyu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

"Wizara inatambua uhitaji mkubwa wa majosho katika maeneo mbalimbali nchini na katika mwaka wa fedha 2022/23 wizara itaendelea na ujenzi wa majosho katika maeneo yenye uhitaji yakiwemo ya jimbo la Ikungi,"alisema.




Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA



Mbunge wa Monduli, Fred Lowassa akiwa ameongozana na Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Tanga, Mhandisi Mwanaisha Ulenge, wakati wakiingia bungeni kuhudhuria mkutano wa saba wa Bunge la Bajeti kikao cha kumi, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kusaka fedha miradi umwagiliaji

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha wa 2022/23, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji, itaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo kukamilisha miradi ya umwagiliaji mbalimbali ikiwamo miradi ya Mkoga na Kitwiru.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kutatua kero zinazokabili miradi ya umwagiliaji ya Mkoga na Kitwiru iliyoko Manispaa ya Iringa.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema miradi ya umwagiliaji ya Cherehani Mkoga yenye hekta 750 na Kitwiru yenye hekta 100 inakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa muda mrefu.

Changamoto nyingine, alisema ni kutokamilika kwa miundombinu pamoja na miundombinu kuharibiwa na mafuriko.

Pia alisema serikali itaenda kukarabati miradi ya Mgambalenga na Nyanzwa iliyoko katika wilaya ya Kilolo katika bajeti ya mwaka 2022/23.

Alisema mradi wa Ikweha hadi sasa umetumia Sh. milioni 800 na kwamba serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na utafika kutatua tatizo lililopo ili wakulima wafanye kilimo chao.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, alisema mradi wa umwagiliaji wa Izazi una tatizo la uchakavu wa miundombinu na kuhoji lini serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu hiyo.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema miradi yote ya umwagiliaji imewekewa mpango mkakati katika mwaka wa fedha ujao na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaipitia miradi yote nchini ili kujua inayofanya kazi na inayohitaji marekebisho.

# Wasiojulikana waiba nyaya kwenye transfoma

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) Kahama mkoani Shinyanga, limewatangazia kiama wananchi wanaohujumu miundombinu ya shirika kwa kuiba nyaya aina ya kopa kwenye tansfoma na kuisababishia serikali kuendelea kukosa mapato yake kupitia huduma ya umeme.

Vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa nyakati za usiku na watu wasiojulikana katika maeneo ya Kakola kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala na kata ya Mwendakulima Manispaa ya Kahama na imekuwa ikisababisha wananchi kukosa huduma kwa zaidi ya saa 24.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, Jimmy Monyo, kwa niaba ya Meneja King Fokanya na kuonya kuwa atakayebainika kutenda vitendo hivyo, atashtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi kwa kuwa kufanya hivyo ni kuhujumu shirika kuendelea kutoa huduma ipasavyo. Alisema mpaka sasa transfoma tisa zimeshaondolewa nyaya hizo ambazo huzuiwa transfoma kupigwa na radi wakati wa mvua na kwamba nyaya hizo baada ya kuibwa wanauziwa wanunuzi wa chuma chakavu.

Monyo alitaja baadhi ya maeneo ambayo transfoma zimeharibiwa kuwa ni mtaa wa Mbulu, Mbulu Misheni, Mwendakulima, Mwendakulima Shuleni, Miembeni, kijiji cha Kabale na Kabale Zahanati na sasa mafundi wanaendelea kurejesha nyaya hizo katika transfoma zilizoharibiwa.

"Tumekuwa tukishughulika kila siku kuhakikisha umeme haukatiki katiki mara kwa mara kwa wateja wetu na viwanda vyetu kupata umeme wa uhakika lakini kuna baadhi ya watu wanahujumu shirika kwa kukata nyaya kwenye transfoma. Tukiwabaini watakuwa mfano kwa wengine," alisema.

Monyo aliwataka wananchi kutoa taarifa endapo watamwona mtu nyakati za usiku amepanda juu ya transfoma hata kama yuko na gari la shirika, wafike na kumhoji kwa kumwomba kitambulisho cha kazi na wakati mwingine wapige simu kwa namba za huduma kwa wateja ili kujiridhisha zaidi.

Mmoja wa wateja waliofika TANESCO kupata huduma, Agnes John, alisema wanaohujumu miundombinu ya shirika wamekuwa wakisababisha viwanda vyao kusimama kwa kukosa nishati, hivyo kuiingizia hasara serikali kwa kukosa mapato kupitia huduma hiyo.

Mteja mwingine, Abdullah Juma, alisema kukatika kwa umeme mara kwa mara kunasababishwa na watu wasio waadilifu wanaohujumu miundombinu ya shirika na hiyo imekuwa ikifanya serikali kukosa wawekezaji wakubwa chanzo kikiwa ni wananchi wenyewe, hivyo akashauri hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wanaobainika kufanya hivyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya ACB, Silvest Arumasi (mbele) akishiriki kwenye futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka serikali kutoa msukumo ajira kwa watu wenye ulemavu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imeombwa kutilia mkazo ajira kwa watu wenye ulemavu ikiwamo kuzipa msukumo wizara, taasisi za umma na binafsi kuzingatia suala hilo.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS) Mkoa wa Morogoro, Hassan Mikazi, alisema jana kuwa iwapo serikali itatilia mkazo suala la ajira kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, itasaidia wenye ulemavu kupata ajira na kujikimu kimaisha.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria hiyo, bado serikali, taasisi za umma na binafsi zimekuwa zikipuuza kipengele kwamba kila penye wafanyakazi kuanzia 20, panapaswa kuwa na asilimia tatu ya watu wenye ulemavu. Alisema jamo hilo ni kinyume cha sheria na linarudisha nyuma maendeleo ya wenye ulemavu wenye elimu licha ya kusoma kwa shida.

Mikazi alisema TAS kwa sasa inatekeleza mradi wa miezi mitatu wa ajira jumuishi kwa watu wenye ulemavu, unaofadhiliwa na Shirika la Habari la Internews inayolenga kuhamasisha jamii husika kupitia vyombo vya habari kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu sawa na watu wengine kwa kuzingatia sheria.

Alisema kila mtu mwenye ulemavu, mwenye sifa za kuajiriwa, anapaswa kupata ajira sambamba na mazingira ya kazi kuwa rafiki kwao na kwamba mradi utatumia njia mbalimbali kuhamasisha jamii vikiwamo vyombo vya habari, mitandao ya kijamii mikutano na watu wenye ulemavu na waajiri kuwaelimisha waifahamu sheria na kuitekeleza ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata ajira na kujikimu kimaisha.

Alisema serikali bado haijaweka msukumo wowote kusimamia sheria hiyo na kwamba ikisimamiwa vizuri itasaidia watu wenye ulemavu waliojitahidi kupata elimu kutobaguliwa na kufikiwa na matangazo ya ajira yanapotoka kwa njia mbalimbali ili wapate ajira walizokusudia.

"Matangazo mengi hayawafikii hasa wale wasioona sababu yanatoka kwenye vyombo vya habari hasa magazeti na yeye (asiyeona) hadi kulipata na kulisoma ni changamoto. Anapokuja kwenye suala la ajira bado wengi waliosoma wako mitaani na hali ngumu ya kiuchumi ya kimaisha kwao," alisema.

Mmoja wa watu wenye ulemavu wa wasioona, Godfrey Omari, aliomba serikali kuona umuhimu wa kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu katika ajira sambamba na kuwaongezea mshahara itakayowarahisishia kukabiliana na changamoto ikiwamo kununua mahitaji yao muhimu.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Morogoro, Oscar Changala, alisema kuna watu wenye ulemavu wenye ajira ya wasio na ajira ambao hawajihusishi na makundi ya watu wenye ulemavu jambo linalotokana na kukosa kujitambua na kusababisha kukosa fursa sahihi kwao.

Alisema program ya ajira jumuishi inaweza kusaidia watu wenye ulemavu katika kupata ajira pale itakapotiliwa mkazo na kuondoa tabia iliyozoeleka ya watu wenye ulemavu kukaa vijiweni licha ya kuwa ni watu waliosoma.

# Wafamasia walaani wamiliki maduka ya dawa kuajiri vishoka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA cha Wafamansia Tanzania (PST), kimelaani vitendo vya baadhi ya wamiliki wa maduka ya dawa muhimu, kuweka watu wasio na taaluma kwenye maduka hayo na kutoa huduma kwa wananchi jambo ambalo ni hatari kiafya.

Katibu Mkuu wa PST, Benson Katundu, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kutokana na baadhi ya video ambazo zimesambaa mitandaoni, zikionyesha baadhi ya maduka ya dawa muhimu yakitoa huduma kupitia watu wasio na taaluma.

Alisema kutokana na video hizo kuonyesha udhaifu huo, PST inalaani tabia hiyo ya wamiliki wa maduka ya dawa muhimu, kuajiri watu wasio na taaluma ya dawa na kuhatarisha afya za wananchi, ikiwamo kupata ulemavu na hata kusababisha kifo.

"Katika mitandao mbalimbali ya kijamii, zimeonekana video kadhaa zikionyesha watoa huduma wasio na taaluma ya dawa wakihudumia katika maduka ya dawa kinyume cha miongozo, sheria na taratibu zinazosimamia maduka ya dawa muhimu na wengine ni wafanyakazi wa ndani tu jambo ambalo ni hatari.

"Chama cha Wafamasia Tanzania tunakemea na kulaani vikali vitendo hivyo vya maduka ya dawa muhimu kuajiri watu wasio na taaluma ya dawa kwani ni hujuma kwa afya za Watanzania. Dawa isipotumiwa kwa usahihi huwa inageuka kuwa sumu mwilini na kusababisha ulemavu hata kifo," alisema. Alisema chama hicho kinaliomba Baraza la Famansia kuangalia upya mifumo ya ukaguzi wa maduka ya dawa muhimu nchini kote yaliyoko mijini na vijijini ili kubaini maduka ambayo yanatoa huduma za dawa kinyume cha taratibu na kuyachukulia hatua ili kuokoa afya za wananchi.

Pia aliwataka wafamansia kila halmashauri waongeze weledi wa kusimamia uanzishwaji wa maduka ya dawa muhimu katika maeneo yao na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha yanahudumiwa na wataalamu wenye sifa. Baadhi ya wananchi wa Shinyanga, waliiomba serikali kudhibiti tatizo hilo la maduka ya dawa muhimu kuajiri watu wasio na taaluma ya dawa, ili kunusuru afya za watumiaji hasa katika maeneo ya vijijini ambako wako wengi.



# Waziri ahamasisha uandishi riwaya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara itatenga bajeti kwa ajili ya mtu yeyote kuandika riwaya na itakayoshinda, uchapishaji wake utagharamiwa na wizara hiyo.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jijini hapa jana alipokutana na wawakilishi wa mwandishi wa kitabu cha Hesabu cha Darasa la Saba kilichoandikwa kwa kutumia mitaala ya Kenya, Uganda na Tanzania, David Inzofu.

"Tunataka kusaidia waandishi ambao wanataka kuandika riwaya. Tunaposema elimu yetu tunataka iakisi mahitaji ya nchi yetu na utamaduni wetu. Tungependa pamoja na wanafunzi kusoma vitabu vya nje, wasome pia vilivyoandikwa na Watanzania," alisema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda alisema lengo la kufanya hivyo ni kuona kunakuwa na Watanzania wengi wanaojitokeza kuandika vitabu.

Alimwagiza Kamishna wa Elimu kuhakikisha kitabu hicho kinapitiwa na wataalamu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili kama kuna sehemu ya kuboresha ifanyike ili kumsaidia mwandishi huyo kuongeza hamasa kwa Watanzania wengi zaidi kuandika vitabu na kuhamasisha usomaji.

Pia alisema kumekuwapo na maoni ya kutumia Kiswahili kufundishia katika siku zijazo, hivyo kunahitaji maandalizi ili kufika huko, Watanzania wenyewe waandike vitabu, uwezo na uzoefu wa kutafsiri vitabu vya Kiingereza kuwa vya Kiswahili.

"Tungependa kukuza Kiswahili na hii inahitaji maandalizi, hivyo lazima kuwe na vitabu vingi vya Kiswahili, huwezi kuanza kutumia lugha ya Kiswahili huku vitabu vikiwa vya Kiingereza. Huyu Mwalimu David Inzofu nafurahi kwamba ametafsiri hiki kitabu kwa Kiswahili itabidi tumsaidie ili Baraza la Kiswahili lihakiki kitabu hicho," alisema Waziri Mkenda.

Mmoja wa wawakilishi wa mwandishi wa kitabu hicho, Novatus Makunga, alimshukuru Waziri Mkenda kwa kukubali kupokea nakala hizo kwa ajili ya kuvipitia na kwamba inaonyesha nia njema ya serikali iliyo nayo kushirikiana na wadau wengine wa elimu katika kuendeleza kuboresha elimu nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati alipofuturu na watoto wenye mahitaji maalum wa kituo cha Buigiri kinachomilikiwa na Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

# Wanaokaidi kuvisha mifugo hereni waonywa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema wafugaji wanapaswa kutambua suala la kuvisha hereni mifugo si hiari bali ni lazima kwa sababu lengo la kufanya hivyo ni kupanua soko la mifugo ndani na nje ya nchi, ikiwemo kufuga kwa tija.

Pia Waziri Ndaki amezitaka halmashauri na wafugaji kuchukua tahadhari, kutokana na matarajio ya uwapo wa uhaba wa malisho kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ili wasiuwe mifugo kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Akizungumza wakati wa mkutano maalumu wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) jana, uliokwenda sambamba na uzinduzi wa uvishaji hereni mifugo, Ndaki alisema wafugaji wanapaswa kuzingatia suala la kuvisha hereni katika mifugo yote badala ya kuweka chapa, ili kuendana na soko la dunia.

Wafugaji, alisema wakifanya hivyo itawasaidia kutambua mifugo yao hata ikipotea kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa sababu watakuwa na hereni ambazo ni utambulisho wa mifugo kutoka eneo fulani.

"Nawaomba wafugaji zingatieni suala la kuvisha hereni mifugo yenu. Hii itawapa urahisi wa kuitambua pale inapopotea na hereni zitavishwa kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe," alisema Ndaki.

Alisema baada ya uzinduzi wa uvishwaji hereni, wafugaji wanapaswa kuwa tayari kuvisha hereni kwenye mifugo na kuondokana na dhana ya kupiga chapa wanyama ikiwamo kufuga kwa mazoea.

Kuhusu tahadhari ya uwapo wa uhaba wa malisho kwa mifugo, alisema halmashauri na wafugaji wanapaswa kuchukua kwa kurasimisha maeneo waliyo nayo ambayo yatawasaidia kuandaa mashamba

ambayo watahifadhi malisho.

Alisema wafugaji kuhifadhi malisho ni muhimu sana kwa sababu kipindi cha kiangazi kunakuwa na uhaba wa malisho na kusababisha migogoro baina ya wafugaji na wakulima kutokana na mifugo kuingia katika mashamba ya wakulima.

Kwa mujibu wa Waziri, maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji lazima yarasimishwe ili yajulikane ni ya wafugaji jambo ambalo

litachangia kupunguza migogoro kwa wafugaji na kuongeza kuwa ikitokea yamevamiwa ni rahisi serikali kuingilia kati.

Ndaki alisema serikali iko katika mpango wa kuanzisha mashamba darasa kwa wafugaji ikiwamo kuwapa elimu ili nao wakatoe kwa wafugaji wengine. Alisema anaamini mkakati huo utafanikiwa kuwa na malisho ya kutosha kuliko kutumia mashamba ya serikali pekee.

Awali Mwenyekiti wa CCWT, Jeremiah Wambura, aliwataka wafugaji kutoa ushirikiano kwa serikali pale wanapohitaji kufanya maboresho ya ufugaji wanaofanya ili kusonga mbele.

## Asisitiza bajeti kuzingatia jinsia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Caspar Mmuya, amesema serikali itaendelea kusimamia uandaaji wa bajeti unaozingatia jinsia kama sehemu ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mmuya alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya uandaaji wa bajeti zinazozingatia usawa wa kijinsia ili kuwajengea uwezo wakurugenzi na wakuu wa vitengo kutoka ofisi hiyo.

Alisema elimu hiyo itasaidia watendaji kuzingatia utengwaji wa bajeti zenye mlengo wa kijinsia kama hatua ya mapambano dhidi ya ukatili.

Alifafanua kuwa uzingatiaji wa bajeti zinazogusa jinsia ni muhimu kwa wakati huu ambao wizara mbalimbali zinawasilisha makadirio yao katika Mkutano wa Bunge la Bajeti unaoendelea hatua ambayo itakasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza.

"Tuko kwenye hatua ya kupeleka bajeti zetu bungeni na baadaye kuridhiwa na Bunge lakini kwenye bajeti hizi yawezekana kuna eneo muhimu sana ambalo limeguswa kwa kiasi kidogo na jicho la kuangalia bajeti zetu," alisema.

Pia alibainisha kuwa mafunzo hayo ni muhimu na yamefanyika wakati mwafaka kwa watumishi wa ofisi hiyo huku akizipongeza taasisi na mashirika yanayoiunga mkono serikali kusimamia usalama wa wananchi na kulinda haki za binadamu utakaochochea ustawi wa raia na taifa kwa ujumla.

Mwezeshaji kutoka Sekretarieti ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Joel Mangi, ambaye pia ni Mchumi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, alitaja baadhi ya sababu za kuendelea kwa matukio ya kikatili ndani ya jamii kuwa ni umaskini hasa kwa wanawake.

Chanzo kingine, alisema ni ukosefu wa elimu, mila na desturi kandamizi wanapokuwa hawajitegemei kiuchuni inachochea ukatili ndani ya familia.







Mwandishi wa gazeti hili, Rahma Suleiman, akitoa damu kupima malaria katika kituo cha Afya Kidimni nje ya mji wa Zanzibar jana, wakati wa ziara ya waandishi wa habari waliofika kituoni hapo, kujua hali halisi ya ugonjwa huo, iliyoandaliwa na shirika la misaada la Marekani USAID na Kituo cha Kudhibiti na Kujikinga na Magonjwa (CDC) kwa kushirikiana na kitengo cha Malaria Zanzibar (ZAMEP). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mama mwinyi asisitiza sadaka mwenzi mtukufu wa Ramadhan

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, amewataka wananchi kuendelea kuimarisha ibada na kutoa sadaka kwa wingi katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ambao una mahitaji mengi.

Mama Mariam aliyasema hayo kwa nyakati tofauti wakati akitoa sadaka ya futari kwa wajane, wazee na wenye hali ngumu katika kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja. Alifanya hivyo pia kwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 70 wa kisiwa cha Uzi mkoa wa Kusini Unguja.

Mama Mariam ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, alisema mwezi mtukufu wa Ramadhan ndio uliosisitizwa kukithirisha ibada sambamba na kutoa sadaka. Alisema katika kumi la mwisho la mwezi mtukufu wa Ramadhani, ni vyema waumini wakaongeza ibada pamoja na visimamo vya usiku ili kuupata usiku wenye cheo.

Akizungumza na wananchi, wajane, wazee na wenye hali ngumu katika shehia nne za Tumbatu, alisema jumuiya yake imeamua kuwapelekea sadaka wananchi hao kutokana na mahitaji waliyo nayo.

Alisema Zanzibar Maisha Bora Foundation imekuwa ikitoa misaada kwa makundi mbalimbali katika jamii wakiwamo kinamama, watoto, wazee, wasichana, wajane na wale wenye hali ngumu kwa ajili ya kufikia azma iliyowekwa na jumuiya hiyo.

Mama Mariam alitoa wito kwa wale wote wenye uwezo kuendelea kutoa sadaka zao kwa wale wasiokuwa na uwezo hasa katika kipindi hiki cha mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alimpongeza Mama Mariam na jumuiya yake kwa misaada yake hiyo ikiwamo vyakula kwa kinamama 110 pamoja na misahafu kwa ajili ya misikiti na madrasa za kisiwa hicho. Ayoub alisema hatua aliyoichukua Mama Mariam ya kutoa sadaka kwa wananchi wote bila kujali tofauti zao za kisiasa ni ya kupongezwa na kuungwa mkono kutokana na imani yake ya kujali mahitaji ya watu wa makundi yote.

Pia alipongeza juhudi zinazochukuliwa na wananchi wa Tumbatu katika kujiletea maendeleo bila kujali tofauti zao za kisiasa jambo ambalo limekuwa likiutia moyo uongozi wa mkoa kwa kutambua kwamba siasa zina muda wake.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar, Tabia Makame, alimpongeza Mama Mariam kwa uamuzi wake huo wa kuwafikiria wajane wa Tumbatu na kwenda kuwapa sadaka ya futari katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya kinamama hao, Sheha wa Shehia ya Tumbatu Jongoe, Miza Ali Sharif, alizipongeza juhudi hizo na kueleza furaha yao kwa jinsi alivyowajali na kuwathamini.

# Nyumba 62,900 zafikiwa anwani za makazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NYUMBA 62,880 zimesajiliwa Mkoa wa Kusini Unguja, katika mpango wa anwani za makazi na postikodi lililoanza Machi 12, mwaka huu, sawa na asilimia 96.1.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa huo, Rashid Hadid, alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Tunguu, mjini Unguja, kuhusu maendeleo ya suala hilo.

Alisema kati ya nyumba hizo, wilaya ya Kati zilizosajiliwa ni 41,200 na wilaya ya Kusini 22,264, huku lengo likiwa kusajili nyumba 66,011. Pia alisema mkoa huo kwa sasa umeanza uwekaji wa namba za barabara na tayari njia 1,551 zimeshasajiliwa na kufuatiwa na uwekaji wa namba za nyumba. Alisema dhana nzima ya uwekaji wa mfumo wa anuani za makazi na Postikodi nchini licha ya kuwa ni utekelezaji wa sera ya taifa ya postikodi ya mwaka 2003, ni maelekezo ya kimataifa ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na Umoja wa Posta Duniani (UPU) na ilani ya CCM 2020 - 2025.

"Ni jukumu la kila mwananchi kulinda, kuitunza na kutumia vyema miundombinu ya anwani za makazi na postikodi kwa kutambua na kuthamini umuhimu wake wa kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na serikali kwa maendeleo ya taifa.

Pia alisema pamoja na kuwapo kwa changamoto mbalimbali katika kazi hiyo, suala hilo kwa mkoa wao limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutunza miundombinu na kutoa rai kwa wale wananchi ambao watahitaji kubandika namba kwa mujibu wa maelekezo ya serikali wanatakiwa kufika katika ofisi zao kupatiwa maelekezo na utaratibu wa kuweka namba katika majengo yao.

# Kikwazo kumaliza malaria chaelezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema licha ya Zanzibar kufanikiwa katika mapambano dhidi ya malaria, bado kuna changamoto zinazozuia kumaliza kabisa malaria ikiwamo maambukizi kwa wasafiri.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya Malaria duniani ambayo kilele chake huadhimishwa Aprili 25 ya kila mwaka.

Mazrui alisema lengo kuu la serikali ni kufikia zero malaria ifikapo mwaka 2023 na kwa sasa imebakia asilimia moja kufikia mafanikio hayo kutokana na juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali ya Zanzibar ikishirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za kitaifa na kimataifa.

"Napenda niwatanabahishie kuwa pamoja na ugonjwa huu kupungua sana, bado upo hapa Zanzibar kama takwimu za mwaka 2021 zinavyotuonyesha kuwa ni wagonjwa 6,096 ndio walioripotiwa na kudhibitishwa kuwa na ugonjwa wa malaria. Kati ya hao wanawake walikuwa 2,377 (asilimia 39) na wanaume walikuwa 3,719 sawa na asilimia 61," alisema huku akibainisha kuwa watoto walikuwa 549 sawa na asilimia tisa.

Alisema ugonjwa wa malaria kwa wasafiri wa ndani (Unguja/Dar es Salaam, mikoani Tanzania Bara/Unguja bado ni changamoto inayohitaji msaada mkubwa hasa kutokana na Zanzibar kuwa na bandari nyingi zisizo rasmi.

Kwa mujibu wa Waziri, takwimu kutoka Wizara ya Afya zinaonyesha kuwa kati ya wagonjwa 6,096 walioripotiwa mwaka 2021, 4,145 sawa na asilimia 68 walikuwa na historia ya kusafiri nje ya Zanzibar kutoka katika maeneo tofauti ya Tanzania Bara.

Waziri Mazrui alisema kwa mwaka 2021, vifo vinne viliripotiwa kutokana na ugonjwa wa malaria na Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinakaribia kumaliza malaria kwa mujibu wa muongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Muhammed Haji kutoka Kitengo cha Malaria Zanzibar, alisema wagonjwa kutoka nje ya Tanzania ambao hugundulikana na malaria wanapoingia Zanzibar, ni kutoka Kenya, Congo, Comoro na Burundi lakini kiwango chao ni chini ya asilimia mbili.



CAREEN

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI APRILI 23, 2022



# NDANI YA BOKSI Rihanna, Diamond lazima uwapende

UNADHANI itakuaje pale Rihanna akionekana karibu na mwanamuziki wa Tanzania, Diamond Platnumz wakitumbuiza jukwaani?

Ni wazo zuri, lakini linahitaji muda kumuona Rihanna ambaye ni maarufu Marekani na visiwa vya Barbados, wakifanya ngoma kali pamoja.

Hata hivyo, Diamond amesema ndoto hiyo itatimia hivi karibuni kwani kila kitu kinaenda vizuri, ikiwamo mazungumzo ya kufanya kazi pamoja katika wimbo mmoja.

Diamond akizungumza na BBC, amesema ni jambo jema kufanya kazi ya kimataifa na Mwanamuziki mkubwa duniani.

Nyota huyo amesema si jambo rahisi kumpata mwanamuziki huyo na kukubali kufanya naye kolabo, lakini amefanikiwa kumshawishi mpaka akakubali.

“Ningependa kufanya kazi na Rihanna, nahisi itakuwa ni ngoma kali sana, kama sio kwenye album hii basi inayofuata, tumeshaongea na Rihanna na timu yake, kila kitu kipo sawa, kwa mambo yanayoendelea anaweza akawepo kwenye album hii au ijayo” amesema.

BASI SAWA

## Afande Sele ni kweli lakini?



IMEKUWA si bahati kwa mdogo wake Afande Sele, kwani kabla ya kifo cha Maunda Zorro, kufariki walipeleka mahari kwa Mzee Zahir Zorro kwa ajili ya kumposa.

Kupitia Planet Bongo ya East Africa Radio Afande Sele, amesema anachojua yeye ni miongoni mwa familia yake kwani angekuwa hai hadi sasa mdogo wake angemuoa.

"Maunda Zorro mimi ni familia yangu, mahari yake nimepeleka kwa Mzee Zorro na Banana Zoro, tukawakabidhi pesa tukisubiri harusi lakini kwa bahati mbaya Mungu kafanya kazi yake". Amesema

## Wellu 'usingo maza' usikupe kiburi



MWIGIZAJI wa filamu Wellu Sengo maarufu kama 'Matilda' amesema hawezi kumzungumzia mzazi mwenzake Steve Nyerere, kwa sababu anamlea mtoto peke yake.

"Mimi ni mzazi nina watoto wawili wa kike, siwezi sana kumzungumzia mtu kama hayupo katika maisha yangu.

Mtoto ni wa kwangu mimi ni 'single mother' sina ugomvi na mtu," amesema Matilda

Amesema mabinti zake wawili wanamfariji kila siku, anachokifanya sasa ni kuwajengea misingi ya maisha yao wasije kupata tabu.



## Careen hakuwa mchepuko wa Barakah

MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Careen Simba, amemtuhumu Naj kuwa chanzo cha yeye kuachana na Barakah The Prince, wakati akiwa mjamzito.

Careen ambaye pia ni mpambaji wa video za muziki, amesema amejuana na Barakah muda mrefu na hakuwa kama mchepuko kama inavyodaiwa na watu.

"Mimi na Barakah tulijuana muda mrefu sana, mimi mpaka nabeba mimba tukaachana na Barakah na kuzinguana kwa sababu ya Naj, sikuwa mchepuko nilikua mwanamke wake". Amesema.

## Shimo la kifo: Kazikwa asiyehusika

**Na Adam Fungamwango**

AMETENDWA, ameumizwa, amedanganywa, sasa ameamua kuua. Ameamua kumuua mwanaume yoyote atakayekutana naye mbele.

Mavazi yake na ukatili wake alionekana kama ni mnyama. Lakini ni binadamu. Binadamu akikasirika na kuvurugwa anakuwa zaidi ya mnyama.

Hii ni filamu ya 'Shimo La Kifo', iliyochezwa na kina Zainabu Fundi, Isa Kombo, Khamisi Kumianga, Dorah Martin, Meshark Antony, Salim Ketembo na wengineo.

Ni kama mzimu kwenye kijiji hicho. Wanaume walianza kupotea. Lakini ukweli ni kwamba walikuwa wanauawa na kuzikwa kwenye shimo lililochimbwa na muuaji. Yalikuwa ni mauaji ya kukusudia. Yanayofanywa na muuaji huyo mwanamke.

Cha ajabu siku moja alikutana na mwanamke. Huyo hakumuachia 'Sina ubaya na wanawake, mimi naua wanaume tu, lakini wewe sitokuachia, nakuweka kwenye kundi la wanaume, akamuua na kumtupa kwenye shimo lile lile.

Walitokea pia vijana wawili, akamuua mmoja, mmoja akapiga kelele kuwa amsamehe kwa sababu wamekwenda kijiji kile kumtafuta baba yao mzazi Amani Yahaya, kwani waliambiwa na mama yao kuwa anaishi kijiji hicho.

Muuaji kwanza alikaa chini. Akamuuliza kijana yule yeye ni nani, akamjibu anaitwa Bakari Yahaya, akamwambia hata aliyemuua anaitwa Issa Yahaya na ni mdogo wake.

Muuaji kwa mara ya kwanza akaanza kulia na kumuomba msamaha. Ndipo alipomwambia Bakari kuwa yeye ni dada yao na anaitwa Shamila Yahaya, kwani huyo mzee anayemtafuta ni baba yake mzazi pia. Akaanza kumsimulia chanzo cha kugeuka mnyama.

Kwanza akamwambia baba yao alifariki na kuacha mashamba mengi na mali, ambazo alimuandikishia mwanaume mmoja anaitwa Makanjila.

Shamila alimuamini mumewe na kumkabidhi kila kitu, lakini mwisho wa siku, akamfumania yupo na shoga yake.

Kibaya zaidi mume alimtimua Shamila na kumchukua shoga yake ndiyo akawa mkewe, huku akiendelea kumiliki mali zote kwa sababu aliandikishwa yeye.

Hiyo ilimvuruga Shamila na kukimbilia porini. Akajenga kibanda chake porini na kuanza kulipa kisasi. Kisasi chake kikawa ni kwa kila mwanaume atakayemuona. Yule mwanamke aliyemuua alikuwa ni shoga yake ambaye aliingilia penzi lake.

Alisikitika sana kumuua mdogo wake Issa, lakini mwishoni akamuua mumewe Makanjia na kumtupa kwenye shimo alilochimba.





## Pamela amtamani Shusho

Mwanamuziki wa Injili, Pamela Tumaini amesema anatamani uimbaji wa Chritisina Shusho, kutokana na kuwa wa kipekee nchini.

"Ninavutiwa na Shusho, ninatamani kufanya kama yeye, nitajitahidi ili iwe hivyo katika nyimbo zangu ninazoendelea kuziandaa ukiwamo wa 'Suprise na Pigana Nao'," amesema Pamela.

Pamela amesema kwa sasa amekuja na mtindo wa kurekodi wimbo mmoja baada ya mwingine hadi akamilishe albamu. Amesema alikuwa kimya kwa muda mrefu na sasa amekuja na nguvu baada ya kuona soko la muziki wa Injili limekua.



## MWENDO WA KAZI NA KUJIRUSHA TU

**Na Adam Fungamwago**

MIAKA ya 1970 hadi 1990 mwanzoni, Tanzania ilikuwa na bendi za Mashirika ya Umma, Makampuni, mpaka Jumuiya za chama. Mfano Juwata Jazz ilikuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi chini ya Chama cha Mapinduzi, na Vijana Jazz, ilikuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Vijana ya Chama cha Mapinduzi.

Leo tunaziangalia bendi zilizokuwa zikimilikiwa na Mashirika ya Umma. Ni kwamba bendi hizo zilikuwa na baadhi ya wanamuziki ambao walikuwa ni wafanyakazi wa mashirika hayo. Ni wachache tu ndiyo walikuwa wanapiga muziki tu.

Wanamuziki waliokuwa na vipaji vya kazi zingine, kusomea au uwezo, walipewa kazi kwenye mashirika hayo, huku wakipiga muziki.

**UDA Jazz Band 'Bayankata'**

Vuta picha konda na dereva wa daladala au mabasi ya UDAT unayoyaona leo, wakimaliza kazi zao za kutwa nzima watoke hapo kwenda kupiga muziki. Na siku zingine wanakwenda kwenye mazoezi, wakimaliza wanaingia mzigoni kuendesha mabasi na kutoza nauli abiria kama kawaida.

Ndivyo ilikuwa kwa bendi ya Uda Jazz. Ilikuwa na wanamuziki wengi ambao ni madereva wa mabasi ya abiria, makonda, mafundi gereji, mafundi wa taa za magari na mengineyo.

Mfano mtunzi wa vibao vya 'Tulele Tuboe' na 'Nenda Kaishi Salama', Mikidadi Seif ambaye alifariki katikati ya mwaka 2000, alikuwa ni kondakta wa mabasi ya UDA. Hamza Kalala yeye alikuwa fundi wa taa za magari. Ilikuwa ni bendi maarufu sana nchini na kurekodi nyimbo nyingi zilizopendwa kama hizo zilizotajwa hapo juu. Zingine ni 'Nachunga Heshima' na 'Sakina Kaharibu Masomo'.

**National Panasonic Band**

Hii ilikuwa ni bendi ya kiwanda cha kutengeneza redio pamoja na betri maeneo ya barabara ya Pugu jijini Dar es Salaam.

Haikuwa maarufu sana, na haikudumu muda mrefu sana, lakini ilikusanya wanamuziki mahiri na kutoa baadhi ya vibao vilivyotamba sana.

Vibao kama 'Fahari ya Macho' na 'Tofiki' ambavyo vilitesa sana kwenye anga la muziki wa dansi hadi leo hii.

**Biashara Jazz Band**

Ni bendi iliyokuwa inamilikuwa na Kampuni ya Biashara za Ndani. Ilikuwa ikiongozwa na Juma Ubao maarufu kama 'King Makusa'.

Nayo pia haikuwa maarufu sana kwa jina, kuliko hata kiongozi wa bendi hiyo, King Makusa ambaye alikuwa maarufu zaidi. Nyimbo maarufu zaidi za bendi hiyo ni 'Posa Nitaleta', 'Kipini cha Dhahabu', na nyingine nyingi.

**Bima Lee 'Magnet Tingisha'**

Shirika La Bima la Taifa ndilo lilikuwa likiimiliki bendi hii na haikuwa bendi ya muziki tu, bali hata kundi la taarabu. Ilikuwa ni moja kati ya bendi kubwa kabisa nchini, iliyozitikisa bendi kubwa kama Msondo Ngoma na Sikinde Ngoma ya Ukae.

Iliweza kuchukua wanamuziki kadhaa kutoka Sikinde kama Joseph Mulenga, Abdallah Gama, Suleiman Mwanyiro, Shaaban Dede na wengineo. Ni bendi iliyokuwa na nyimbo nyingi sana maarufu kama 'Makulata', 'Baba Shani' na nyinginezo.

**Tancut Almasi Orchestra**

Awali ilisemekana kuwa ni bendi iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha kukata almasi mkoani Iringa, lakini baadaye ilikuja kubainika kuwa bendi hiyo ilikuwa ikimilikiwa na wafanyakazi wa kampuni huyo kama wao na si kampuni yenyewe ya kuchonga na kukata almasi.

Ni moja kati ya bendi kubwa zilizotikisa nchini Tanzania, na wimbo wake maarufu zaidi ni 'Masafa Marefu.'



# Card B amuanika mtoto wake

RAPA mkali wa kike Cardi B na mume wake Offset, wametoa rasmi picha ya mtoto wao wa pili.

Picha hiyo ambayo waliiweka katika ukurasa wao wa Instagram, inamuonyesha mtoto huyo akiwa amevishwa nguo yenye taji la manyoya kichwani.

"Nawashukuru kwa kila mtu ambaye ameniombea mimi na familia yangu, Nawapenda na nawakumbatia kila familia yenye watoto nawatakia maisha mema." Ameandika Card B.



## Ritam, Anosike wafunga ndoa ya kimila

MWIGIZAJI filamu kutoka Nollywood, Rita Dominicis, hatimaye amefunga ndoa ya kimila na mume wake Fidelis Anosike.

Rita na Anosike walioana April 19 katika jimbo la State na shughuli yote ya harusi ilifanyika kulingana na mila ya kabila la Imo.

Picha zilizosambaa mitandaoni zilimuonyesha msanii huyo akiwa na marafiki zake waliohudhuria sherehe hiyo.

## JJC Skillz mtoto hapigwi na bakora

RAPA mkongwe wa Nigeria Abdul Bello, maarufu kwa jina la JJC Skillz, amefuta picha zote za mtoto wake Benito kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Hatua hiyo inakuja baada ya shutuma zilizotolewa dhidi yake na mama wa mtoto huyo, Mella ambaye amemshutumu nyota huyo wa muziki kwa kumpiga mwanawe na kumdhuru mwili.

Bella aliweka ujumbe mtandaoni "Wakati unajionyesha kwenye mitandao ya kijamii ukijifanya kuwa mcha Mungu bandia lakini ni muhusika mkuu katika hadithi ya kutamanisha, mtoto uliyemshambulia na kumdhuru bado anapata nafuu kutokana na majeraha aliyoyapata mwilini,"






## Rihanna, ASAP wana jambo lao

MWANAMUZIKI kutoka Marekani Barbados, Rihanna anadaiwa ana matatizo na mpenzi wake A$AP Rocky, kiasi cha kuelekea kuachana.

Kulingana na mtandao wa PageSix, vyanzo vinaeleza wawili hao wameonekana kuwa tofauti na wakati wowote wanaweza kuweka wazi.

Chanzo kingine kimesema Rihanna na ASAP walionekana katika mitaa ya Craig huko West Hollywood wiki iliyopita wakitembea katika hali ya mashaka tofauti na zamani.

## Vreezy Ville azidi kupeta na MEGA SUPA

STAA wa kizazi kipya kutoka Cameroon, Vreezy Ville, amewashukuru mashabiki kwa mapokezi makubwa ya ngoma yake mpya 'MEGA SUPA' inayofanya vizuri kwenye mitandao.

Vreezy amesema wimbo huo unatia moyo na kuonyesha nguvu ya Mungu katika kubadilisha maisha ya mtu kutoka chini mpaka juu.

"Kazi hii nzuri ya sanaa inajumuisha sauti nzuri, Rhythmz na ngoma za Kiafrika ambazo zitakufanya ucheze na ufurahie baraka za Mungu pamoja nasi. Ni wimbo unaogusa rika na vizazi vyote ndio maana mapokezi yamekuwa makubwa ndani na nje ya Cameroon, ," amesema Vreezy Ville.



# KWAHERI MWAI KIBAKI

## ■Aliingia Ikulu na kuinua uchumi wa Kenya
## ■Ghasia, mauaji 2007 yalimnyima usingizi

**Na Mwandishi**

**ALIYEKUWA rais wa tatu wa Kenya, Mwai Kibaki amefariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa akiwa na umri wa miaka 90.**

**Rais Uhuru Kenyata, ametangaza kifo hicho kupitia runinga mbalimbali nchini Kenya na kutangaza yataandaliwa mazishi ya kitaifa ya kiongozi huyo.**



KATIKA taarifa yake, Uhuru amemuelezea hayati Kibaki kama kiongozi aliyeinua uchumi , demokrasia na kuimarisha vipato vya raia wa nchi hiyo.

Aidha, Rais Kenyata, alimtaja kama kinara wa kupatikana kwa katiba mpya ya mwaka 2010 na kuongoza uidhinishaji wake.

Alisema bendera zote katika ofisi za umma , wizara na balozi zote duniani zitapepea nusu mlingoti hadi pale shughuli ya mazishi itakapokamilika.

**SAFARI YA MWAI KIBAKI KISIASA**

Aliingia siasa mapema wakati Kenya ilipopata uhuru wake mwaka 1963 na alifanya kazi katika nyadhifa mbalimbali serikalini .

Baada ya kuhudumu kama makamu wa rais, alijipatia uzoefu na maarifa ya kisiasa katika uongozi na kumfanya kutoyumba wakati alipokalia kiti cha urais nchini humo.

Kibaki alianzisha chama chake cha Democratic Pary DP baada ya kutofautiana kisiasa na aliyekuwa rais wa pili wa Kenya, Daniel Toroitich Arap Moi, hapo ndipo alipoanza safari yake ya kuwania nafasi hiyo ya juu.

Baada ya kuchukua madaraka alionekana kama mtu aliyeleta mabadiliko mapya nchini humo, akiwa kiongozi aliyechaguliwa kidemokrasia akiungwa mkono kitaifa na kimataifa.

Huku utawala wake ukizongwa na masuala ya ufisadi, Kibaki alianzisha mabadiliko ya kikatiba , kuleta elimu ya msingi ya bila malipo na kufanya juhudi kuinua sekta ya afya iliyozorota .

**WAPI CHIMBUKO LAKE?**

Mwai Kibaki alizaliwa Novemba 15, 1931, akiwa mtoto wa mwisho katika familia ya watoto wanane wa Kibaki Githinji na mkewe Teresia Wanjiku.

Akiwa mzaliwa kutoka kabila kubwa la Wakikuyu , aliishi katika kijiji cha Gatuyaini katika kaunti ya Nyeri.

Alionyesha uwezo wa kipekee katika masomo yake ya msingi katika shule ya upili ya Man'gu, moja ya shule bora nchini Kenya mwaka 1947 hadi 1950.

Matokeo mazuri yalimsaidia kupata ufadhili wa masomo ambapo alijiunga na Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda ambapo alisomea Uchumi, sayansi ya kisiasa na historia.

Uongozi wake ulionekana alipokuwa mwenyekiti wa muungano wa wanafunzi katika chuo kikuu cha Makerere kabla ya kuhitimu na shahada 1955.

Baada ya kuhudumu kama naibu meneja wa kampuni ya mafuta ya Shell nchini Uganda, Mwai Kibaki alipata ufadhili wa kusoma katika chuo cha uchumi cha London.

Alihitimu na shahada ya Uchumi na ufadhili wa umma{ Public Finance}, na alitarajiwa kutumia maarifa yake nchini mwake aliporudi 1958.

**KUINGIA KATIKA SIASA**

Mwaka 1960, alijiunga na chama cha Kenyan African National Union (KANU) na kuwa miongoni mwa wapigania uhuru wa mwanzo wa taifa hilo.

Baada ya mabadiliko kadhaa miaka michache, alisaidia Kenya kujipatia Uhuru wake kutoka kwa Uingereza na miaka mitatu baadaye Mwai Kibaki, alikuwa mwanasiasa mahiri.

Mwaka 1963, alichaguliwa katika bunge la Kenya na kuendelea kuhudumu katika nyadhifa tofauti hadi alipoteuliwa kuwa waziri wa fedha na mipango ya kiuchumi na Rais wa kwanza, mzee Jomo Kenyatta.

Baada ya kujipatia uzoefu na kujiwekea sifa nzuri katika miaka yake ya kwanza katika siasa na serikali, Kibaki aliteuliwa kama Makamu wa Rais chini ya uongozi wa Rais Daniel Arap Moi mwaka 1978.

Licha ya kuwa makamu wa rais, pia alikabidhiwa wizara ya Fedha.

Kama waziri wa fedha, alianzisha mikakati na mabadiliko ambayo yaliiletea Kenya maendeleo.

Mwaka 1982 alikabidhiwa wadhfa wa waziri wa masuala ya ndani.

Mwaka 1988 mgogoro kati yake na Rais Moi, uliibuka baada ya kuchukua madaraka yote na kumuondoa Kibaki kama makamu wa rais, kisha kumpeleka katika wadhfa wa waziri wa Afya.

Tofauti ya kimawazo kati ya Moi na Kibaki ilipelekea msomi huyo wa chuo kikuu cha Makerere kujiuzulu kutoka KANU mwaka 1991.

Baada ya kuchukua hatua hiyo, aliamua kuanzisha chama chake cha Democratic Party (DP) .

Hata hivyo utawala wa Moi ulionekana kushindwa kuhimili vuguvugu la mabadiliko na kusababisha upinzani kuwa mkali dhidi ya uongozi wake.

Vyama vya upinzani viliamua kuungana ili kutoa nguvu moja ambayo ingemuondoa Moi madarakani.

Kibaki alijiunga na viongozi wengine waliokuwa upinzani kama vile Raila Odinga, Michael Kijana, Wamalwa na Charity Ngilu na kuunda muungano wa upinzani ulioitwa National Rainbow Coalition (NARC).

Kibaki alichaguliwa kuwa mgombea wa urais wa Muungano huo na mwaka 2002, alishinda na kuingia Ikulu.

Ushindi wake ulikaribishwa kwa nderemo na matumaini makubwa ya kuboreka kwa maisha ya usoni ya Wakenya.

Alifanya mabadiliko muhimu ya kiuchumi wakati wa muhula wake wa kwanza kama rais.

Hata hivyo jinamizi la ufisadi ambalo Kibaki alikuwa ameahidi kukabiliana nalo wakati wa kampeni zake za uchaguzi lilionekana kumuandama.

Baadhi ya viongozi wa upinzani ambao waliungana naye walidai kwamba Kibaki aliienda kinyume na makubaliano yao.

Raila Odinga na viongozi wengine walibadilika na kuwa mwiba katika serikali ya Kibaki na kumfanya rais huyo kuwafuta kazi.

Hatua yake ilipelekea kuundwa kwa upinzani ambao ulimtoa kijasho katika uchaguzi wa urais wa mwaka 2007 uliokumbwa na utata na ghasia za baada ya uchaguzi.

Katika ghasia hizo watu 1000 walidaiwa kuuawa baada ya upinzani ukiongozwa na Raila Odinga kuandamana kupinga matokeo yake.

Kufuatia ghasia hizo jamii ya kimataifa ikiongozwa na mpatanishi mkuu Koffi Annan , akishirikiana na marais wa Tanzania Marehemu Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete waliingilia kati na hatimaye wakabuni serikali ya muungano ambapo Raila Odinga aliingia serikalini kama waziri mkuu.

Na baada ya muhula wake kukamilika 2013, alimwachia madaraka Uhuru Kenyatta, aliyeibuka mshindi wa uchaguzi mkuu wa urais mwaka huo.

# Makampuni, mashirika yalitamba enzi hizo

## •Ugawaji, Chibuku, MECCO, Mwatex



Mabaki ya Jengo la Kampuni ya Kusindika Nyama Tanganyika Packers maeneo ya Kawe, jijini Dar es Salaam.

**Na Adam Fungamwango**

ULIKUWA ni wakati wa Ujamaa. Wakati ambapo Makampuni na Mashirika yote yalimilikiwa na Serikali.

Njia Kuu za uchumi zote zilimilikiwa na serikali. Hii ilikuwa ni baada ya Azimio la Arusha kutangazwa mwaka 1967.

Rais wa Awamu ya Kwanza Nchini, Julius Kambarage Nyerere alileta kusudio la kutaka serikali kumiliki njia kuu za uchumi.

Ndipo alipopitisha azimio hilo kwenye mji wa Arusha (sasa jiji) mwishoni mwa Januari mwaka 1967 na alilitangaza Februari 5 mwaka huo huo.

Katika misingi yake alikusudia kulinda Uhuru wa Taifa, lakini sio tu Tanzania, bali na mataifa ya jirani ambayo kwa wakati ule yalikuwa katika tawala za kikoloni, misingi yake ililala katika ukombozi wa Afrika na Taifa na kufanya kuwa watu wa taifa huru pasina kuingiliwa na mabepari.

Pili ilikuwa kurudisha mali zote zilizokuwa zinamilikiwa na mashirika binafsi kuwa mali za serikali, maarufu kama mali ya umma zitakazomilikiwa na wakulima na wafanyakazi.

Kwa kutambua umuhimu, serikali ilihimiza wanachi kufanya kazi kwa bidii na kuzuia wanyonyaji.

Kiini cha Azimio la Arusha kilikuwa ni kupambana na kila aina ya udhalimu wa kibepari, unyonywaji, kunyanyaswa, kukandamizwa, kushushiwa utu, kudharaulika na kutengwa.

"Tumeonewa kiasi cha kutosha. Tumenyonywa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliosababisha tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa.Sasa tunataka Mapinduzi. Mapinduzi ya kuondoa unyonge, ili tusionewe tena na tusipuuzwe tena".

Yalikuwa ni baadhi ya maneno maarufu kwenye hotuba ya Mwalimu Nyerere wakati wa Azimio la Arusha.

Ni maneno yaliyonukuliwa na kutungiwa nyimbo nyingi za dansi na taarabu wakati huo ambazo zinaendelea kutamba mpaka sasa.

"Kuonewa, na kupuuzwa na kunyanyaswa kweli wananchi." Ni moja kati ya nyimbo za bendi ya DDC Mlimani Park, Sikinde Ngoma ya Ukae.

"Mabepari walia, mabepari walia, kukatiwa mirija, walipotangaziwa, walipotangaziwa Azimio la Arusha." Ni mmoja wa wimbo maarufu sana uliokuwa unaimbwa kwenye halaiki, shuleni na sherehe mbalimbali.

Sidhani kama kuna mzee, kijana au mtoto wa kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1960, ambaye anaishi hadi leo asiujue wimbo huu.

Hapo ndipo nchi ilipoanza kwa kutaifisha mali za mabepari ambazo walikuwa wamejilimbikizia, pia kuanza kuanzishwa makampuni na kujengwa viwanda mbalimbali.

Ndipo vilipokuja Viwanda, Mashirika na Makampuni mengi ambayo baadhi yaliondokea kuwa maarufu sana na hadi leo hii yamebaki kumbukumbu kwenye vichwa na Watanzania wengi.

Yalianza kufa kwenye miaka ya 1990 baada ya kuanza kushindwa kujiendesha, na yakawa yanaleta hasara.

Kuna sababu nyingi, ikiwemo kuwa na wafanyakazi wengi kuliko uwezo wa kuzalisha, ingawa sitaki kwenda ndani sana kwa hilo.

Mengine yalibinafsishwa na sasa yapo mikononi mwa watu binafsi. Yapo ambayo serikali imeingia ubia na watu binafsi, maarufu kama wawekezaji.

Machache sana ndiyo bado yanamilikiwa kwa asilimia mia moja na serikali, mfano Shirika la Ugavi wa Umeme, TANESCO.

Hebu tuyakumbuke baadhi ya Makampuni na Mashirika hayo.

Kwanza kabisa kulikuwa na kampuni maarufu ya kusindika nyama iliyokuwa maeneo ya Kawe, Dar es Salaam, Tanganyika Packers, halafu likawa na samaki, TAFICO, kukawa na Shirika la Usafiri Dar es Salaam, UDA, halafu yale ya kusafirisha abiria mikoani ilikuwa ni Kamata, huku makampuni ya kusafirisha mizigo na bidhaa mikoani kukawa na KAURU, KAUDO na mengine mengi ambayo yalibadilika majina tu kutokana na mikoa husika. THB ilikuwa ni benki ya nyumba Tanzania, pia kulikuwa na General Tyre, kiwanda cha kutengeneza matairi cha jijini Arusha.

Kulikuwa na viwanda vya nguo kama URAFIKI, KILTEX, MWATEX, Sunguratex na vingine vingi.

Tunaikumbuka piaTanzania Wood Industry Co ltd (TWICO), Agricultural and Industrial Supplies Co Ltd (AISCO) na Building Hardware and Electrical Supplies Co Ltd (BHESCO).

Vile vile kulikuwa na, Shirika la Meli za Mwambao Tanzania (TACOSHILI), UFI, CO-CABS, na kiwanda cha kutengeneza redio cha National Panasonic na kile cha Arusha, Philips.

Dodoma kulikuwa na DOWICO, yaani Dodoma Wine Company, Shirika la Bima la Taifa, NEDCO, Shirika la Usafiri la Taifa (NTC), KIOO LIMITED, SUDECO, Posta na Simu, NBC, NACO, NARCO, BBH, National Cold Chains Operations (NCCO), maarufu kama Chakula Barafu, kampuni ambayo ilikuwa inauza nyama pori, pamoja na samaki wa maji baridi, pia kulikuwa na Kampuni ya Viatu Tanzania maarufu kama BORA, RTC, DARTEX, DABCO, TISCO, ZZK ya Mbeya, Tuncut Almasi ya Iringa na Amboni Plastic ya Tanga.

Kwa kumalizika mada hii hatuwezi kulisahau Shirika la Ugawaji la Taifa, maarufu kama UGAWAJI.

Kwa sababu baada ya vita ya Kagera, kulitokea uhaba wa chakula nchini kuanzia miaka ya 1980, hivyo watu wengi ni lazima walikumbuke shirika hilo kwa sababu ndiyo lilikuwa na kibali cha kusambaza vyakula madukani kama unga, mchele, sukari, na bidhaa zingine ambazo zilipatikana kwa tabu sana.

Pia kulikuwa na kampuni moja ya kutengeneza kinywaji au pombe ya CHIBUKU, ambayo nayo ilikuwa ni moja kati ya makampuni maarufu sana wakati huo, hadi katikati ya miaka ya 1990.

**Tuma meseji 0716 350534.**



Sergey Lagovskiv (26) akimkumbatia Ludmyla Verginska (51) wakati wakiomboleza kifo cha rafiki yao Igor Lytvynenko, ambaye aliuawa na wanajeshi wa Russia katika jengo ambamo walijificha eneo la Bucha, **PICHA: REUTERS**

# Russia yazidi kusonga mbele vita Ukraine

## ■Donbas, Mariupol zazidi kudhibitiwa
## ■Rais Ukraine ajigamba kurudisha maeneo

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amejigamba kwamba mafanikio ya Russia katika eneo la mashariki ya nchi hiyo ni ya muda, kwani vikosi vyake vitarudishwa nyuma hadi mpakani.

Alitoa matamshi hayo katika hotuba yake ya hivi karibuni kwa taifa.

"Kusini na mashariki mwa taifa hilo, watekaji wanaendelea kufanya kila kitu kuonyesha wana kitu cha ushindi. Wanaingiza wanajeshi katika ardhi yetu. Pia wanajaribu kuwasambaza katika maeneo waliyoteka,"

Aliongeza "Hakuna hata hatua moja kati ya hizi zitasaidia Russia katika vita dhidi ya taifa letu. Wanaweza kuchelewesha muda ambao wavamizi watalazimika kuondoka nchini mwetu lakini wataondoshwa."

Vikosi vya Russia viliwakamata wanakijiji 42 mashariki mwa Donetsk siku ya Alhamisi, lakini Ukraine ilisema itavikomboa.

**WIKI CHACHE ZIJAZO ZITAKUWA MUHIMU**

Hatma ya Donbas kuanguka inategemea jinsi pambano linalondelea kwa wiki mbili au tatu zijazo, amesema mtaalam wa kijeshi Justin Crump.

"Ndio maana kipindi hiki ni muhimu sana kwa kuzingatia hilo, utaona amani katika migogoro, au vita vya muda mrefu vinavyoendelea, hiyo inategemea pande zote mbili bila shaka," alisema.

Alisema itategemea jinsi Warussia watakavyokabiliana na Ukraine , kama Putin atakubali kile alichonacho wakati huo, ikiwa wanahisi wameharibu kitovu cha jeshi la Ukraine na kuonyesha vifaa vya Nato havitoshi kuwazuia - wanaweza kuendelea kuchukua miji kama Kharkiv.

Alisisitiza Russia bado wana vikosi 22 vya vita kaskazini mwa Kyiv na Belarus, wanazuiliwa huko kwa sababu, inaweza kufanya uchaguzi wake kuwa wazi kwa nchi nzima, lakini hiyo inaweza kuwa ngumu ikiwa itapoteza nguvu nyingi huko Donbas.

**PICHA ZA SATELAITI ZAONYESHA MAKABURI YA HALAIKI**

Makaburi ya pamoja ya wakazi wa Mariupol waliouawa na jeshi la Russia katika kijiji kilicho karibu na bandari ya kusini mwa Ukraine yamegundulika.

Katika taarifa iliyopatikana kupitia picha za Setelaiti zilionyesha watu wakichimba mitaro ya urefu wa mita 30 na kutumia malori ya kubeba taka kuleta miili ya watu kwa ajili ya kuzikwa.

Mauaji hayo yamefanyika katika eneo lililo nje kidogo ya kijiji cha Manhush, magharibi mwa jiji lililozingirwa pwani ya Azov.

Halmashauri ya jiji la Mariupol, imechapisha picha ya angani zinazodaiwa kuonyesha makaburi hayo.

Tovuti hiyo ilisema "mitaro ni mikubwa mara mbili ya makaburi ya hivi karibuni".

Hata hivyo, kampuni ya teknolojia ya Marekani Maxar ilisema kwamba picha zake za hivi karibuni za satelaiti zenye kiwango cha juu zinaonyesha kuwepo kwa eneo la kaburi la watu wengi kwenye ukingo wa kaskazini-magharibi mwa Manhush nchini Ukraine.

"Mapitio ya picha zetu za satelaiti kutoka katikati ya Machi hadi katikati ya Aprili yanaonyesha kuwa wigo wa seti mpya ya makaburi ulianza kati ya Machi 23 hadi 26 mwaka huu na umeendelea kuongezeka katika wiki kadhaa zilizopita,"

Iliongeza "Makaburi yamepangwa katika sehemu nne za safu za mstari na mapya zaidi ni 200,"

Kampuni hiyo ya Marekani pia imechapisha msururu wa picha za satelaiti zinazodaiwa kuonyesha eneo la kaburi la watu wengi karibu na Mariupol.

**PUTIN BADO YUKO KATIKA NAFASI YA USHINDi**

Maofisa wa nchi za Magharibi wanasema wanaona baadhi ya ishara kwamba Russia inashughulikia baadhi ya matatizo yaliyoikumba wiki za mwanzo za uvamizi wake nchini Ukraine.

Walisema hao wanajaribu kuboresha zaidi kwenye safu yake kama vile kwenye upande wa kutoa amri na kudhibiti mashambulizi.

Lakini maofisa hao walisema Warussia bado wanafanya kazi katika misafara mirefu kwenye barabara moja, ambayo ina maana kwamba wanasalia katika hatari ya kushambuliwa.

Walisema wanajeshi wa Ukraine, huendelea kupigana kwa busara zaidi na kwa njia nzuri.

Baadhi ya njia za mawasiliano za Russia bado ni ndefu hasa kusini kutoka Kharkiv na zinakabiliwa na mashambulizi kutoka magharibi.

Maofisa walisema Rais Vladimir Putin bado yuko katika nafasi ya kushinda, na matokeo kadhaa yanayowezekana, ambayo hakuna hata moja wanayotarajia kuona yakitokea haraka.

Mataifa ya Magharibi yanajiandaa kuendeleza uungwaji mkono wa kijeshi kwa Ukraine kupitia kipindi kirefu cha vita.

Kampeni ya Russia yenye mafanikio katika Donbas inaweza kusababisha kutazamwa upya baadhi ya malengo yao ya kabla ya vita, kama vile Kyiv na Odesa.

Walieleza kwamba vikosi vya Russia vinapata mafanikio takribani mara tatu au moja kwa idadi dhidi ya jeshi la Ukraine, lakini inategemea jinsi Russia inavyotumia vikosi hivyo kwa ustadi na uwezo.

Maofisa walisema iwapo Putin anataka kuifunga Mariupol, hii haitakuwa kazi ndogo na itaendelea kuzuia uwezo wa vikosi hivyo kushiriki katika operesheni huko Donbas.

Walisema kuwa matumizi ya Russia ya makombora ya masafa marefu ya Iskander yamepungua kwa kiasi fulani katika wiki iliyopita, na ina wasiwasi kuhusu viwango vya utumiaji na uwezo wa kuhifadhi silaha tena.

**MAREKANI YAAHIDI KUPELEKA SILAHA**

Rais wa Marekani ametangaza kutuma silaha nyingine zenye thamani ya dola milioni 800 za kurusha makombora kwenye maeneo ya juu.

Pia msaada huo unajumuisha risasi 144,000 na ndege zisizo na rubani zitakazotumika kwenye uwanda tambarare mashariki mwa Ukraine.

Silaha zingine zilizotumwa kufikia sasa ni pamoja na ndege zisizo na rubani za Switchblade ambazo zinaweza kugeuzwa kuwa mabomu ya kuruka na silaha za kuzuia ndege zinazoweza kurusha helikopta kutoka angani.

Kwa jumla, zaidi ya dola bilioni tatu ya msaada wa kijeshi imetumwa kwa Ukraine tangu Russia ilipovamia Februari 24, mwaka huu.

"Wakati mwingine tutazungumza kwa upole na kubeba mkuki mkubwa, kwa sababu tunatuma wengi walio ndani pia," alisema Biden akimaanisha silaha za kukinga mizinga.

Zaidi ya hayo, Pentagon ilisema Alhamisi kwamba inaipa Ukraine ndege zisizo na rubani sawa na uwezo wa Switchblade.

Ofisa wa Pentagon anasema silaha hizo zilitengenezwa kwa haraka na Jeshi la Wanahewa ili kukabiliana na mahitaji ya Kiukreni.

Aina na uwezo mahususi wa 'drones ghost', hata hivyo, haujulikani hadharani. Marekani hadi sasa imekuwa ikisita kutuma vifaru kwa Ukraine vilivyotengenezwa na Marekani.

Aidha, wakati Marekani hadi sasa imejitolea kupeleka Ukraine helikopta 16 za aina ya Mi-17, haijatuma moja kwa moja ndege nchini Ukraine na imeeleza mpango wa kutuma ndege za Mig-29 zilizotengenezwa na Soviet kutoka nchi nyingine.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHARLES KATEBI BULUBA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 660 DGT – DAIHATSU.** Chassis namba **S200P0019547.** Engine namba **EF7401479.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/150454/2022.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 12 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MUSSOLINI ELIAKIMU MSHANGA**

**PROSPER ELIMRINGI MSHANGA...............WAOMBAJI**

**EDWARD ELIBARIKI MSHANGA....WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki kwa marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 09 mwezi 06 mwaka 2022
Imesainiwa dar es salaam leo tarehe 21 mwezi 04 mwaka 2022

NAIBU MSAJILI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ROTARY CLUB OF ARUSHA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA HILUX PICK UP yenye USAJILI NAMBA T669 ANR, CHASSIS NAMBA: LN8500085546 na ENGINE NAMBA:212803072. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: ARU/ARU/158312/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

LAURENT KADORIN LAURENT Anatangaza kupotelewa kwa Kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 779 CSJ CHESESIS NA. MD6M14PA9L4G07480 Engini namba AK414907299 Yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi au Piga simu 0687838225 MOR/MOR/R-B/157936/2022

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAIRICE J. NGATUNGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo (Diploma in Secondary Education). Chenye namba **E0618-0002** kilichotolewa na Baraza la Mtihani wa Taifa kwa mtihani wa mwaka 2015 katika chuo cha **AGGREY CHANJI TEACHERS' COLLEGE.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi namba **IRI/IRI/RB/93836/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAIRICE J. NGATUNGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita. Chenye namba **S0681-0542** kilichotolewa na Baraza la Mtihani wa Taifa kwa mtihani wa mwaka 2013. katika shule ya **IVUMWE SECONDARY SCHOOL.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi namba **IRI/IRI/RB/93833/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI**

**(MCA/84)**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**NAMBA YA SHAURI MADAI YA GHARAMA (Taxation cause)**

**Na.1/2022**

**MLETA MAOMBI 1. FLORENT KYOMBO 2. FRANCISCA KYOMBO**

**MJIBU MAOMBI: ANDREW ALOYCE**

**Kwa ENDREW ALOYCE-Mjibu maombi**

**Kwa kuwa mdai/mdaiwa/ameleta/wameleta/maombi yake/yao kwamba MAOMBI YA MADAI YA GHARAMA**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatano tarehe 4/5/2022 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu maombi hayo.

Angalia kama hukuudhuria siku hiyo iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 20/4/2021.

Hakimu Mkazi
Dodoma


---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAPPYNESS GOSBERT MATAMBULA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(TOYOTA PASSO)** yenye namba za usajili **T 343 CTB** Chassis namba: **KGC100037973** Injini namba: **IKREAA7973** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/109804/2022.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



LAURENT JIGGE anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 3861/0160 kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari ANDERLEK RIDGES mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA: DAR/MAG/RB/575173/2021

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**

**Wilaya ya Morogoro kituo cha Kingolwila**
**Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirath Na 4....2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU AMINA ISSA KAPEMBA WA KINGOLWIRA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SELEMANI HARUNA MRISHO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27/04 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 12/04/2022**

---

**Notice/summons to appear (O.v.r.20(1) of (CPC)**
**(Substituted service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**( LAND DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**EXECUTION NO.63 OF 2020**

**(Arising from Land Case No. 381 of 2015)**

**ALKARIM SHAMSHUDIN HABIB...............**
**APPLICANT/ DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**EDWIN KAIJAGE NDYAMUKAMA.........**
**1ST RESPONDENT/JUDGMENT DEBTOR**

**LIBERTY INTERNATIONAL LIMITED........**
**2ND RESPONDENT/JUDGMENT DEBTOR**

**TO:**
**LIBERTY INTERNATIONAL LIMITED...............2ND RESPONDENT/JUDGMENT DEBTOR**

**WHEREAS:** The above named applicant has instituted an applicationagainst you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **09th day of May, 2022 at 09:00hrs before Hon. W.A. Hamza (Room NO.8)** to answer the said application; and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support your defence.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**Given under my hand and the seal of this court, this 21st day of April 2022**

DEPUTY REGISTRAR

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUDI YASINI IDD,** Anatangaza kupotelewa kwa Cheti cha kuzaliwa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0385/0106** Kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ujiji mwaka 2016 yeyote atakaye viona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0719099461**
**MOR /MOR/RB/159394/2022**

---

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-2

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Mpaka hapo Siwatu hakujua nini tena afanye kwa mtu yule. Msaada gani mwingine anaotakiwa kufanya. Aliishiwa mbinu. Kama mtu yule angalau angekuwa anaongea hata kwa mbali, wangeweza kujadiliana nini cha kufanya. Akafikiri kidogo. Angalau sasa wasiwasi ulianza kumuondoka baada ya kugundua hakukuwa na hatari yoyote kama ambavyo yeye na wenzake awali walivyodhani.

"Samahani, basi naomba kwenda kijijini nikawaambie watu kama kuna mtu ili waje wakusaidie, sawa ee?" Siwatu alimwambia mtu yule.

Akaitikia kwa kichwa kukubali. Siwatu aliinua ndoo yake na kujitwisha. Asingeweza kujitwisha kwa urahisi kama ingejaa, lakini kwa wakati huo ilikuwa imebaki nusu.

Aligeuka na kumtazama yule mtu. Naye akainua tena mkono kama ishara ya shukurani. "Nitarudi, usiwe na wasiwasi." Alisema kwa sauti, akimtia matumaini.

**********************

"Kaka Dibwela, kaka Dibwela kuna mtu kule porini njiani karibu na barabara." Alipiga kelele huku akitweta. Ni baada ya kurudi nyumbani kwake na kutua maji yake nusu yaliyosalia baada ya kumwagia mtu yule na kumnywesha.

"Nani wewe, mtu gani Siwatu?"

"Twende, twende kaka atakufa yule." Akazidi kusisitiza.

"Nini wewe?

"Kuna mtu wamempiga kule, wamemtupa, anahitaji msaada."

"Kwani unamjua?"

"Simjui."

"Sasa kama humjui wewe anakuhusu nini?"

"Kaka Dibwela, hivi yule mtu akifa, halafu serikali, siyo hii ya kijiji chetu, ile ya juu ikijua hilo, si tutakuwa matatizoni?"

Maneno hayo yalimwingia kidogo Dibwela, akajikuta akiimuuliza tena, "umesema wapi vile?"

"Kule porini karibu na barabara kuu."

"We ulimuona ukiwa peke yako?"

"Tulikuwa na wenzangu, kina Mage na Mpaje." Lilikuwa ni swali la woga. Alionekana kuogopa kwenda peke yake.

"Ngoja nikamwambie Kobelo twende naye."




**Kilichowashangaza Dibwela na Kobelo ni kwamba, Siwatu alikwenda moja kwa moja mpaka alipo majeruhi yule bila kuhofia kitu chochote.**

"Haya."

Walipiga hatua za haraka haraka hadi nyumba ya nne kutoka pale walipo. Kama kawaida nyumba za vijijini huwa zipo mbalimbali kidogo, mara nyingi nyumba moja huwa na eneo ambalo hutumika kama shamba dogo la kulima mazao mbalimbali kama mahindi, mihogo na mengine yanayofanana na hayo.

Ndiyo maana nyumba huwa mbalimbali na si kama za uswahilini ambazo zinakuwa zimekabiriana kama mikate iliyopo dukani.

"Kobelo upo ndani?"

Badala ya sauti ya mtu, kilisikika kikohozi chepesi. Iliashiria kuna mtu ndani.

"Kobelo ugeni wako huu."

Mlango wa bati ukafunguliwa. Na alitoka kijana mmoja mwenye umri wa miaka 26 hivi.

"Kuna nini bwana Dibwela, mbona hivyo? Halafu mbona umeongozana na dada yako, vipi?"

"Bwana ee, dada kaja hapa nyumbani kwangu, kaniambia kuna mtu kama vile amepigwa, yupo hoi anasema, mimi sijamuona, labda yeye akueleze."

"Nani kwani huyo mtu na yupo wapi?"

"Ameumia sana, sijui amepigwa yule, ana majeraha mwili mzima, hawezi hata kuongea na kusimama, anahitaji kusaidiwa."

"Unamfahamu?" Kobelo aliuliza swali kama aliloulizwa na kaka yake.

"Simfahamu, ila kwa sababu yupo kijijini kwetu, nimeona asaidiwe tu."

"Huyu dada yangu huruma zake zingine bwana, kanimbia twende tukamchukue na kumsaidia, ndiyo maana tumekuja hapa ili utusaidie."

"Siyo mbaya, umekwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji?"

"Hapana."

"Kaka zangu, yule mtu ni mgonjwa, yupo kwenye hatari ya kufa, anahitaji kwanza asaidiwe, halafu taarifa apelekewe mwenyekiti, kama tukisema twende kwake, tunaweza kumkuta hayupo halafu turudi tena, tunaweza kumkuta amekufa, sasa tutakuwa tumefanya nini?" Siwatu akadakia.

"Haya, basi ngoja tuchukue machela huku nyuma ya nyumba, twende tukaangalie nini tunaweza kufanya."

Dibwela na Siwatu ni mtu na dada yake wa baba na mkubwa na mdogo.

Ilikuwa ni safari ya kipande kirefu cha njia. Siwatu akiwa ametangulia ili kuwaelekeza sehemu ambayo alimuacha mtu huyo. Walimkuta. Lakini ni kama vile alianza kuzidiwa tena.

Kilichowashangaza Dibwela na Kobelo ni kwamba, Siwatu alikwenda moja kwa moja mpaka alipo majeruhi yule bila kuhofia kitu chochote.

Walichokuwa hawaelewi ni kwamba msichana huyo saa moja na nusu iliyopita alibaki peke yake na majeruhi huyo akamwagia maji kupooza joto na kumtia nguvu, pia akanywesha.

Wenyewe walidhani alimuona, akatimua mbio na kuja kuwaeleza tukio hilo.

Walimuangalia, lakini hawakumtambua. Ina maana alikuwa mgeni kijijini hapo. "Labda ni wa vijiji vya jirani." Dibwela alimwambia mwenzake.

Waliweka machela yao chini. Walimnyanyua kwa uangalifu na kumuweka akilalia machela.

Wote wawili hawakuonekana kulifurahia sana zoezi lile. Walilazimika kwa sababu ya Siwatu. Walitaka kumridhisha, lakini haikuwa ndani ya mioyo yao. Mtu wasiyemjua ametoka wapi na amepatwa na matatizo gani ni ngumu kwao kumsaidia.

Dibwela alikubali kwa sababu hakutaka kumuudhi dada yake. Ni msichana yatima. Alifiwa na wazazi wake wote wawili. Baba yake alifariki miaka minne iliyopita, na mama yake miaka mitatu iliyopita. Na si Dibwela tu ambaye ana undugu naye.

Hata kijijini hapo walimchukulia Siwatu kuwa ni mwanakijiji maalum. Alikuwa na upendeleo maalum, kwani kwenye kijiji hicho haijapata kutokea mtoto wa kike kufiwa na wazazi wake wote wawili akiwa na umri wa miaka 19 tu, tena akiwa ni mtoto pekee.

Kila kitu kilichofanyika kijijini hapo alikuwa na upendeleo maalum. Wazazi wake walimuachia nyumba mbili. Moja ndiyo anaishi yeye na nyingine alimpa kaka yake huyo Dibwela akae.

Mbali na hayo wazazi wake walimuachia mashamba mawili makubwa. Moja lilikuwa la mama yake, na la pili baba yake. Mashamba hayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliyomfanya aishi vizuri, kwani hakuwa na mtu mwingine yoyote anayemtegemea, au kitu chochote cha kuendesha maisha yake.

Alilima, alikodisha watu na kujipatia mazao na pesa. Kwa sasa alikuwa na miaka 23.

Waliinua machela taratibu na kuanza kurejea kijijini. "Tunampeleka wapi?" Kobelo aliuliza.

"Kwangu. Huyu kwanza anatakiwa apate huduma ya kwanza, halafu kama akipata nafuu, anaweza kuondoka, lakini wakati huo tunatakiwa kwenda kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kijiji kuhusu tukio hili." Dibwela akatoa wazo hilo

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# YANGA PRINCESS, SIMBA QUEENS VITA YA HESHIMA

**Na Saada Akida**

MECHI ya marudiano ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kati ya watani wa jadi, Yanga Princess dhidi ya Simba Queens itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam inaonekana ni ya kusaka heshima pamoja na kulipiza kisasi, imeelezwa.

Timu hizo mbili zinashuka dimbani huku Simba Queens wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mabao 4-1 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, ambao ulichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Simba Queens inahitaji kupata ushindi ili kujihakikishia katika mbio za kutetea ubingwa wao ikiwa na rekodi nzuri ya kushinda mechi zote 14 za ligi hiyo msimu huu.

Yanga Princess nao wanahitaji kulipa kisasi na kufuta uteja mbele ya watani zao ambao wamekuwa wakiwaonea kwa misimu mitatu mfululizo.

Simba Queens inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 43 wakati Yanga Princess yenyewe iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 32, kila timu imecheza michezo 14.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma alisema wamejiandaa vizuri na wataingia katika mchezo huo kusaka matokeo mazuri kwa ajili ya kufikia malengo ya kushinda michezo sita ya duru la pili.

**Nkoma alisema mechi ya Simba Queens dhidi ya Yanga Princess ni kubwa na kwa sababu hiyo wataenda kucheza mchezo huo kwa nidhamu kwa sababu hawataki kupoteza malengo yao ya kushinda mechi sita za kwanza za hatua ya lala salama.**

"Naweza kucheza dhidi ya Yanga Princess bila ya hofu kutokana na baadhi ya wachezaji wetu waliokuwepo katika kikosi changu kutokuwepo, kukosekana kwa Oppah haina shida kwa sababu Simba Queens haitegemei mchezaji mmoja," alisema Nkoma.

Nahodha wa Simba Queens, Fatuma Issa alisema wamejiandaa vizuri na wako fiti kuhakikisha kila mechi wanapata ushindi mkubwa.

"Tumeandaliwa vizuri na tunawahakikishia mashabiki wetu tutapata ushindi wa mabao mengi, tunaingia kwa kuwaheshimu na tunaenda kupambana kusaka pointi tatu ili kufikia malengo yetu," alisema Fatma.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema alisema wamejipanga vizuri na watahakikisha wanafanya vyema katika mchezo huo ili kujenga heshima ya klabu.

"Mechi hii tunaenda kutafuta heshima, hatupendi kufungwa na Simba kila msimu na kuifanya Derby iliyokuwa na heshima kwa ligi ya Wanawake," alisema Edna Lema.

Nahodha wa Yanga Princess, Neema Charles alisema :"Tumejiandaa vizuri na benchi la ufundi limemaliza majukumu yao, kazi iliyobaki ni kwetu wachezaji kuhakikisha hatufungwi tena na Simba,".




Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakiwa na watoto wa kituo cha SOS cha Zanzibar baada ya kuwatembelea na kuwapatia misaada mbalimbali ya chakula. Serengeti Girls imeweka kambi Zanzibar kujiandaa na mechi yake dhidi ya Burundi itakayochezwa Mei Mosi, mwaka huu. **PICHA: TFF**

# Azam yajinoa kwa Mafunzo

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuendelea kujiimarisha, Azam FC inatarajiwa kuikaribisha Mafunzo kutoka Zanzibar katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Azam FC inatumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya kuwakabili Geita Gold ambao watakutana Aprili 29, mwaka huu huko mkoani Geita.

Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria alisema mchezo huo utachezwa kwenye uwanja wao wa nyasi asilia ili kuwapa wachezaji nafasi ya kuzoea mazingira watakayokutana nayo huko Geita.

Zakaria alisema timu yao kwa sasa inaendelea vyema na malengo ni kuona wachezaji wanaimarika tayari kwa kazi ya kuchukua pointi tatu kwenye kila mchezo watakaocheza.

"Timu itaondoka jijini Dar es Salaam Aprili 28, mwaka huu kuelekea Geita na matarajio ya kila mchezaji ni kwenda kushinda mchezo huo, tunajua wapinzani wetu pia wanajipanga, lakini kwetu tunasema hakuna kitakachotusimamisha kuvuna pointi tatu," alitamba ofisa huyo.

Aliongeza kikosi chao kimejiandaa kukutana na changamoto mbalimbali kwa sababu wanafahamu mechi zilizosalia ni ngumu na kila timu imejipanga kutimiza malengo yake ya kubakia kwenye ligi hiyo ya juu nchini.

Alisema pia baada ya mchezo huo wataanza safari ya kuelekea Bukoba kufuata wenyeji Kagera Sugar ambao watapambana nao ifikapo Mei 3, mwaka huu.

## Wadau wamlilia marehemu Ntemi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MSANII wa ngoma za kabila la wasukuma ambaye ni mwalimu wa kwanza kufundisha wazungu lugha ya kisukuma, Edward Mashiku Ntemi (69) amefariki dunia.

Marehemu Ntemi anatajwa aliwafundisha wazungu kuimba na kucheza ngoma za kisukuma.

Akizungumza kwa niaba ya familia mtoto wa marehemu, Paulo Lusana, alisema baba yake alifariki Aprili 18, mwaka huu akiwa nyumbani kwake Kisesa Bujora, wilayani Magu jijini hapa kutokana kusumbuliwa na ugonjwa wa kansa.

"Marehemu Edward Ntemi alianza kuugua mwaka 2021 akiwa nchini Denmark, tulimpeleka kupata matibabu na majibu yalionyesha anasumbuliwa na ugonjwa wa kansa ya ini ndipo tulipoamua kumrudisha nyumbani hapo Novemba, mwaka jana na kuendelea na tiba mbadala za miti shamba," alisema Paulo.

Alisema kati ya mwaka 1979/ 1980 baba yake alialikwa kwenda Denmark kwenye kongamano la muziki na alifanya vizuri hadi kuwavutia wazungu.

Mwenyekiti wa Chama cha Mtakatifu Sesilia Bujora, Lucy Sospeter, alisema kifo cha msanii huyo ambaye alikuwa mwalimu wao kupitia ngoma za Bugobhogobho ni pigo.

Naye Mhifadhi wa Makumbusho ya Bujora, Richard Buluma, alisema kifo cha Edward ni pigo kwa kuwa hakuwa mbinafsi.

## Gymkhana Arusha yapania makubwa

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Gymkhana ya Arusha umesema timu yao ya vijana ya tenisi imejipanga kufanya vizuri katika mashindano ya GFA Bridges yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Timu ya vijana ya tenisi ya klabu hiyo, Godluck Mollel alisema maandalizi ya kikosi chake yamekamilika.

"Haya mashindano yatashirikisha wachezaji 25 kutoka Moshi na wenyeji Arusha," alisema Mollel.

Aliongeza lengo la kufanyika kwa mashindano hayo ni kukuza vipaji vya nyota chipukizi ambao watapeperusha bendera ya nchi katika michuano mbalimbali hapo baadaye.

"Tunafuraha kuona sasa hivi watu wengi wanajitokeza kucheza tenisi, imekuwa tofauti na zamani, sasa mchezo unavutia watu kutoka sehemu mbalimbali," kocha huyo alisema.

Kocha huyo alisema kupitia mashindano hayo watapata wachezaji wazuri wa timu ya taifa kwa ajili ya kushiriki michuano ya kimataifa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED KUUZA SITA

MANCHESTER United huenda ikawauza, Marcus Rashford, Anthony Martial, Aaron Wan-Bissaka, Eric Bailly, Phil Jones na Alex Telles mwisho wa msimu huu kama mpango wa mabadiliko chini ya mkufunzi mpya, Erik ten Hag. (***Sun***)

### HAG AMTAKA RICE

KIUNGO wa kati wa West Ham na Timu ya Taifa ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 25, ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Erik Ten Hag. (***Guardian***)

### DE BEEK NA MATUMAINI

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kupatiwa fursa ya kufufua matumaini yake ya kupata nafasi Old Trafford kwa ujio wa kocha wake wa zamani wa Ajax, Erik Ten Hag. (***Sun***)

### UNITED KUSAJILI VIUNGO

MLINZI wa kati, viungo wawili wa kati na mshambuliaji ndio watakaokuwa kipaumbele katika dirisha la uhamisho mwisho wa msimu huu kwa Manchester United.(***Sky Sports***)

### MCCLAREN AKATALIWA

MANCHESTER United imekataa ombi la Erik Ten Hag la kumrudisha katika klabu hiyo aliyekuwa kocha msaidizi wa Sir Alex Furguson, Steve McClaren ili kumjumuisha katika makocha wake. (***Telegraph***)

### RB YAMGOMEA NKUNKU

KLABU ya RB Leipzig kwa mara nynegine tena imesisistiza kiungo mshambuliaji, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, atabakia kuwa mchezaji wao msimu ujao, licha ya kuwaniwa na klabu za Manchester United na Arsenal. (***Sky Sports Germany***)

### LUKAKU ANUKIA MILAN

AC Milan huenda ikamwania mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28. (***Goal***)

### PAGE KUTUA BURNLEY

KLABU ya Burnley inalenga kumsajili kocha wa muda wa Wales, Rob Page mwenye umri wa miaka 47 msimu huu ili kuchukua nafasi ya Sean Dyche. (***90Min***)

### SPURS, EVERTON VITANI

EVERTON imejiunga na Tottenham Hotspur katika mbio za kumwania golikipa wa Timu ya Taifa ya England na Westbrom, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 29. (***Mirror***)

### GUIMARAES ANUKIA MADRID

REAL Madrid inamchunguza kiungo wa kati wa Newcastle na Timu ya Taifa ya Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 24. (***AS***)

### YILMAZ ATAKIWA SPURS

MLINZI wa kushoto wa klabu ya Besiktas na Uturuki, Ridvan Yilmaz mwenye umri wa miaka 20, analengwa na Tottenham Hotspur na klabu kadhaa za Ulaya. (***TRT Spor***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: ILIKUWA LAZIMA BARCA KUPATA USHINDI

## ●●●Ingawa kocha huyo afunguka hajafurahishwa na kiwango...

**BARCELONA,** Hispania

USHINDI wa Barcelona dhidi ya Real Sociedad kwenye Uwanja wa Real Arena Alhamisi usiku ulikuwa "muhimu kwa mustakabali wa klabu", kwa mujibu wa Xavi.

Pierre-Emerick Aubameyang alifunga bao pekee katika mchezo huo ambao Barca ililaza Real goli 1-0, na kujivuta hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, La-Liga.

Lilikuwa ni jaribio la pekee la Blaugrana hao kulenga goli katika mchezo mzima na walimiliki mpira kwa asilimia 44.3, kiwango chao cha pili kuwa chini zaidi tangu msimu wa 2005-06 - na umaliziaji mbaya kutoka kwa Alexander Sorloth na Alexander Isak ukawaruhusu Barca kuondoka na pointi zote tatu.

Barca sasa hawajafungwa katika mechi 13 zilizopita za ugenini za La-Liga, ambao ni mbio zao bora zaidi tangu Aprili mwaka, 2019.

Xavi alifurahishwa na ukweli kwamba ushindi wao ulikuja dhidi ya mpinzani wa nne bora, hata kama uchezaji wao ulikuwa mbali na alivyokuwa anataka.

"Nimeridhika na pointi tatu. Ni muhimu na muhimu kwa siku zijazo kwa timu na klabu. Ni ushindi wa dhahabu," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Lakini sijaridhishwa na mchezo, kipindi cha kwanza, ndio, lakini kipindi cha pili tuliteseka, lazima tuwe wakweli na kujikosoa, hatujakuwa wazuri. "Lazima tuboreshe. Hii sio njia. Haukuwa mchezo wetu bora. Hizi ni pointi tatu muhimu dhidi ya mpinzani wa moja kwa moja wa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ni mchezo ambao nimeteseka zaidi, pamoja na ule dhidi ya Villarreal. Tuliona uchovu."

Gerard Pique na Jordi Alba walicheza baada ya kuonekana kupata majeraha ya misuli na kuashiria mabadiliko, huku Ronald Araujo akitolewa nje kwa tatizo la goti na Dani Alves pia alionekana kukabiliwa na tatizo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,171,

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.14
X | 3.32
2 | 3.22

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE GEA AFURAHIA UJIO WA TEN HAG



**MANCHESTER,** England

DAVID de Gea "anafuraha sana" kufanya kazi chini ya Erik ten Hag baada ya Mholanzi huyo kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Manchester United, Alhamisi.

Ten Hag atawasili kutoka Ajax mwishoni mwa msimu huu na kuchukua mikoba ya bosi wa muda, Ralf Rangnick kwa mkataba wa miaka mitatu na chaguo la kuongeza mwaka mwingine.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 yuko mbioni kushinda taji la tatu la Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, akiwa na Ajax msimu huu na amesifiwa kwa mtindo wake wa kumiliki mpira.

Aliiongoza Ajax hadi nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19.

De Gea ana furaha hatimaye kuwa na uwazi juu ya mustakabali wa kocha pale United na anatumaini wanaweza kuelekeza nguvu zao katika kutafuta nafasi ya kuingia kwenye nafasi nne za juu za Ligi Kuu England.

"Nimefurahishwa sana na klabu imefanya uamuzi mzuri," alisema De Gea akiiambia tovuti rasmi ya United.

"Tunajua alichofanya kwa Ajax, karibu ameingia fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, alishinda mataji na anakuza wachezaji, kwa hivyo nimefurahia sana.

"Nadhani anacheza mpira mzuri sana. Sasa tunapaswa kuzingatia sana mechi zilizopita lakini tuna shauku ya kujua nani anakuja. Lakini sasa tujikite zaidi kwa Arsenal na kupambana hadi mwisho ili tuwe ndani ya nne bora.

"Ni vizuri kujua na kwa hakika tayari anatazama michezo na kufikiria nini anaweza kufanya ili kuboresha timu, hivyo ni nzuri sana kwetu. Natarajia kufanya kazi chini yake.

# *Hamilton, Serena kuinunua Chelsea*



**LONDON,** England

SIR Lewis Hamilton na Serena Williams wanaripotiwa kuweka pauni milioni 20 kwenye dau la Sir Martin Broughton ili kuinunua Chelsea.

Muungano unaoongozwa na mwenyekiti wa zamani wa Liverpool, Broughton, ambaye ni mojawapo ya mapendekezo matatu yaliyosalia katika mbio za kuwanunua wababe hao wa Ligi Kuu England katika wiki zijazo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sky News, zabuni hiyo imepata msukumo wa hali ya juu huku kila mmoja, Hamilton na Serena Williams akiwa tayari kufadhili ofa hiyo.

Ripoti hiyo inadai Hamilton, bingwa wa dunia w mara saba kwenye Formu 1, na mcheza tenisi, Seren wako tayari kuwekeza pau milioni 10 kila mmoja katik mradi huo.

Aidha, inadaiwa majadili no baina ya pande husik yamekuwa yakiendelea kw wiki kadhaa, huku uamu huo ukielezwa ni uamu mzito wa uwekezaji.

Benki ya wafanyabiashar ya Marekani ya Raine Grou inatarajiwa kufanya uamu zaidi kuhusu mchakato k kamilisha ununuzi huo kw wakati ujao, huku miungan ya wanunuzi ikiongozw na Todd Boehly na Stephe Pagliuca na wagombea we gine wawili waliopo katik kinyang'anyiro hicho.

,243,460

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/04/22 | 17:00 | Leicester vs Aston Villa | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 02. 23/04/22 | 17:00 | Hull City vs Reading | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 23/04/22 | 17:00 | Birmingham vs Millwall | 2.78 | 3.08 | 2.53 |
| 04. 23/04/22 | 17:15 | Fuenlabrada vs Ponferradina | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 05. 23/04/22 | 20:30 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.40 | 3.39 | 2.74 |
| 06. 23/04/22 | 21:00 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 07. 23/04/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 08. 24/04/22 | 16:00 | Burnley vs Wolverhampton | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 09. 24/04/22 | 16:00 | Bologna vs Udinese | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 10. 24/04/22 | 16:00 | Metz vs Brest | 2.98 | 3.22 | 2.33 |
| 11. 24/04/22 | 17:15 | UD Ibiza Eivissa vs Las Palmas UD | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 12. 24/04/22 | 18:30 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.73 | 3.22 | 2.48 |
| 13. 24/04/22 | 21:45 | Lazio vs AC Milan | 2.78 | 3.27 | 2.41 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 23/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3012 | Luton Town vs Blackpool | 1.85 | 3.48 | 3.98 |
| 14:30 | 4372 | Arsenal vs Manchester Utd | 2.14 | 3.32 | 3.22 |
| 15:00 | 1572 | KamAZ vs Torpedo Moscow | 4.39 | 3.46 | 1.72 |
| 16:00 | 1338 | Venezia vs Atalanta | 5.78 | 4.38 | 1.47 |
| 16:00 | 2397 | Torino vs Spezia | 1.65 | 3.67 | 4.97 |
| 16:00 | 2815 | Fatih Karagumruk vs Giresunspor | 2.28 | 3.33 | 2.98 |
| 16:00 | 4142 | Geita Gold FC vs KMC | 2.48 | 2.67 | 3.11 |
| 16:30 | 1131 | Greuther Furth vs Bayer Leverkusen | 6.75 | 4.96 | 1.37 |
| 16:30 | 2644 | SC Freiburg vs Monchengladbach | 1.80 | 3.82 | 3.82 |
| 16:30 | 3658 | RB Leipzig vs Union Berlin | 1.49 | 4.17 | 5.95 |
| 16:30 | 3991 | Eintracht Frankfurt vs Hoffenheim | 2.40 | 3.56 | 2.62 |
| 16:30 | 4267 | FC Koln vs Arminia Bielefeld | 1.50 | 4.27 | 5.57 |
| 17:00 | 1038 | Bournemouth vs Fulham | 2.20 | 3.46 | 2.97 |
| 17:00 | 1274 | Partick Thisle vs Dunfermline | 2.19 | 3.21 | 3.16 |
| 17:00 | 2135 | Derby vs Bristol City | 2.05 | 3.32 | 3.42 |
| 17:00 | 2150 | Birmingham vs Millwall | 3.18 | 3.18 | 2.22 |
| 17:00 | 2292 | Swansea vs Middlesbrough | 3.12 | 3.31 | 2.19 |
| 17:00 | 2403 | Peterborough vs Nottingham | 4.85 | 3.81 | 1.63 |
| 17:00 | 2420 | Morton vs Inverness | 2.95 | 3.19 | 2.31 |
| 17:00 | 2758 | Hull City vs Reading | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 17:00 | 2908 | Stoke City vs QPR | 2.03 | 3.33 | 3.47 |
| 17:00 | 3141 | Manchester City vs Watford | 1.12 | 7.33 | 18.31 |
| 17:00 | 4282 | Leicester vs Aston Villa | 2.68 | 3.28 | 2.48 |
| 17:00 | 4332 | West Bromwich vs Coventry | 2.14 | 3.27 | 3.27 |
| 17:00 | 4383 | Sheffield Utd vs Cardiff | 1.56 | 3.87 | 5.56 |
| 17:00 | 4403 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.45 | 3.17 | 2.77 |
| 17:00 | 5252 | Portsmouth vs Gillingham | 1.68 | 3.57 | 4.86 |
| 17:00 | 5577 | Clyde vs Airdrieonians | 4.33 | 3.74 | 1.70 |
| 17:00 | 5709 | Norwich City vs Newcastle | 3.42 | 3.27 | 2.08 |
| 17:00 | 5806 | Queen of South vs Ayr United | 2.91 | 3.21 | 2.33 |
| 17:30 | 4742 | NEC Nijmegen vs Ajax | 11.82 | 6.70 | 1.18 |
| 18:00 | 1412 | FC Krasnodar II vs Veles | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 18:00 | 3381 | Lyon vs Montpellier | 1.33 | 5.38 | 7.17 |
| 18:30 | 4688 | FC Zurich vs FC Sion | 1.54 | 4.30 | 5.20 |
| 19:00 | 2896 | Dodoma FC vs Mbeya City | 3.25 | 2.75 | 2.50 |
| 19:00 | 3106 | Inter vs Roma | 1.60 | 3.97 | 4.96 |
| 19:00 | 3809 | Sochi vs Akhmat Grozny | 1.94 | 3.41 | 3.70 |
| 19:00 | 3853 | Young Africans vs Namungo | 1.36 | 4.30 | 9.60 |
| 19:30 | 2227 | Bayern Munchen vs Borussia Dortmund | 1.35 | 5.55 | 6.34 |
| 19:30 | 2763 | Brentford vs Tottenham | 3.96 | 3.56 | 1.83 |
| 19:30 | 4613 | Malaga vs Eibar | 3.02 | 3.12 | 2.34 |
| 19:45 | 3184 | AZ Alkmaar vs Heerenveen | 1.40 | 4.57 | 6.76 |
| 20:00 | 1771 | St Etienne vs Monaco | 4.17 | 3.72 | 1.77 |
| 20:30 | 1476 | Bursaspor vs Denizlispor | 1.69 | 3.65 | 4.29 |
| 20:30 | 4219 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.33 | 3.34 | 2.89 |
| 21:00 | 2406 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.73 | 3.07 | 2.58 |
| 21:45 | 2373 | Verona vs Sampdoria | 1.72 | 3.72 | 4.37 |
| 22:00 | 4394 | Paris St Germain vs Lens | 1.32 | 5.29 | 7.66 |
| 22:00 | 4609 | Cambuur vs PSV Eindhoven | 8.12 | 5.55 | 1.29 |
| 23:00 | 2380 | Betis vs Valencia | 2.05 | 3.33 | 3.48 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# IHEFU, KITAYOSCE VITANI KUWANIA TIKETI LIGI KUU

**NA CHEJI BAKARI,** MBEYA

TIMU ya Ihefu inatarajia kuwakaribisha Kitayosce kutoka Tabora katika mechi muhimu ya Ligi ya Championship itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, mkoani hapa.

Mechi hiyo ni ya mzunguko wa 26 wa ligi hiyo ambayo inatoa timu mbili moja kwa moja na kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Katika msimamo wa Ligi ya Championship, Ihefu iko nafasi ya pili ikiwa na pointi 53 nyuma ya vinara, DTB ya Dar es Salaam yenye pointi 56 wakati Kitayosce yenye pointi 53 ipo nafasi ya tatu, kutokana na tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa.

**Ihefu inahitaji ushindi wowote leo ili kufikisha pointi 56 na kujiweka katika mazingira mazuri ya kupanda daraja, lakini wakibakiwa na mechi nyingine nne mkononi.**

Mechi nyingine Ihefu watacheza nyumbani ni dhidi ya JKT Tanzania na Pan African wakati watawafuata ugenini African Sports kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga na mchezo mwisho utakuwa ni dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

JKT Tanzania yenye pointi 41 inashika nafasi ya nne na endapo itavuna matokeo chanya kwenye mechi zake zilizobakia, inaweza kuingia katika kinyang'anyiro cha kucheza michezo ya mtoano.

Timu ambazo zinaburuza mkia katika ligi hiyo ni African Lyon yenye pointi 20 na Pan Africans yenye pointi 18.



Wachezaji wa Ihefu SC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Kitayosce kutoka Tabora itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, mkoani Mbeya. **PICHA: MTANDAO**

# Msondo kupamba 'Cheza Kadansi'

**Na Sabato Kasika**

MSONDO Ngoma ni miongoni mwa bendi kubwa ambazo zitatoa burudani katika onyesho la 'Cheza Kadansi' linalotarajia kurindima jijini Dar es Salaam mwezi ujao likihusisha bendi nyingine nne.

Mratibu wa onyesho hilo, Benard James alizitaja bendi nyingine zitakazotumbuiza ni Bogoss Musica ya Nyoshi El-Saadat, Waluguru Original kutoka Morogoro, Mjengoni Classic ya Arusha na Mapacha Watatu ya Jose Mara.

James alisema onyesho hilo ni mwendelezo wa kufufua muziki wa dansi nchini na limekuwa likifanyika katika mikoa mbalimbali, na kwamba mara ya mwisho lilifanyika jijini Mwanza Februari mwaka huu.

Aliongeza itakuwa ni mara ya kwanza kushirikisha bendi ya Msondo tangu onyesho la Cheza Kadansi lianze zaidi ya miaka miwili mitatu iliyopita na wataendelea kushirikisha bendi nyingi na vikundi mbalimbali vya muziki.

"Pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo, muziki wa dansi unaendelea kurejea mdogo mdogo kwenye hadhi yake kama ilivyokuwa zamani, hivyo tunazidi kuandaa maonyesho ya 'Cheza Kadansi'," alisema mratibu huyo.

Aliongeza lengo la maonyesho hayo ni kuhamasisha wadau wa muziki wa dansi kuendelea 'kuusapoti' na pia kushawishi wamiliki wa vituo vya redio na televisheni kuupa nafasi ya kutosha kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# Michezo

Jumamosi Aprili 23, 2022

Nipashe




Xavi: Ilikuwa lazima Barca kupata ushindi

UKURASA 21

## Yanga, Namungo kumaliza ubishi

Na Saada Akida

POINTI tatu ni muhimu. Hii ni kauli kwa makocha wa timu mbili, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze na Kocha wa makipa wa Namungo FC, Josia Steven kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo wa leo, Yanga itawakosa wachezaji wake wawili, Yacouba Songne na Saido Ntibanzokiza huku Namungo FC ikimkosa kipa chaguo la kwanza, Jonathan Nahimana na Blaise Bigirimana.

Kaze alisema kikosi chake kimepata maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo wa leo ambao anaamini utakuwa mgumu, ingawa wamedhamiria kuvuna pointi tatu muhimu.

"Faisal Salum na Khalid Aucho wamerejea na wako fiti kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo), Saido Ntibanzokiza atakosa mechi hiyo kwa sababu hajawa fiti kucheza, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunavunja mwiko wa kupata pointi tatu muhimu dhidi ya Namungo FC," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema wapinzani wao wana kikosi imara na hasa safu ya ushambuliaji ni bora kutokana na kasi nzuri ambayo wanayo na kwa msingi huo watacheza kwa tahadhari na hawatafunguka.

Kaze alisema hatakuwa na mabadiliko makubwa katika kikosi kwa sababu mechi hiyo inaumuhimu mkubwa kuelekea kwenye mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na wapinzani wao, Simba.

"Tumewasisitizia wachezaji wetu kuelekeza akili zao katika kusaka pointi tatu dhidi ya Namungo FC na kusahau kabisa mechi ijayo dhidi ya Simba ambayo iko mbali, tunakibarua kikubwa dhidi ya mpinzani wetu wa kesho (leo)," alisema Kaze.

Naye Josia alisema lengo la Namungo ni moja tu ambalo ni kuvuna pointi tatu muhimu kutoka kwa Yanga.

"Maandalizi yamekamilika kila idara, tuko vizuri na tunatarajia itakuwa mechi nzuri na yenye ushindani, tutaingia uwanjani kwa nidhamu ya hali ya juu ili kutoharibu historia yetu, pamoja na pointi tatu ili kutuweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yetu ya kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa mwakani," alisema Josia.

Nahodha na Namungo FC, Shiza Kichuya alisema wataingia uwanjani kufanya walichoelekezwa na benchi la ufundi ili kupata matokeo mazuri.

"Kazi kubwa imebaki kwetu wachezaji, Yanga ni timu kubwa, tunawaheshimu ila hatuwaogopi kwa sababu tunahitaji kupata matokeo mazuri dhidi yao," alisema Shiza.



Kocha wa makipa wa Yanga, Milton Nienov (katikati), akiwa na walinda mlango wa timu hiyo baada ya kumaliza mazoezi ya kuwakabili Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Simba yatamba kesho ni ushindi*

## ●●● Balozi Sauzi aongoza mapokezi na kuwataka wachezaji wafikirie...

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI kikosi cha Simba kikitua salama Afrika Kusini, Balozi wa Tanzania nchini humo, Meja Jenerali Mstaafu, Gaudence Milanzi amekutana na Ofisa Mtendaji wa Wekundu wa Msimbazi, Barbara Gonzalez na kuwahakikishia watapata ulinzi mkali wakati wote.

Simba iliwasili nchini humo kwa ajili ya mechi ya mkondo wa pili wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates utakaochezwa kesho kwenye uwanja unaomilikiwa na timu hiyo.

Akizungumza kwenye Jengo la Ubalozi la Tanzania nchini humo, Milanzi aliwataka wachezaji wa Simba kuhamishia akili zao uwanjani kwa ajili ya kupata ushindi na kamwe wasiwaze kitu chochote cha nje ya jukumu linalowakabili.

Milanzi alisema maofisa wake wamejipanga imara kuhakikisha mambo yote yanakwenda vyema na wachezaji wafikirie mchezo huo wa marudiano tu.

"Tulikuwa na kikao wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Afrika Kusini kuhusu masuala mbalimbali, tukagusia pia na suala la michezo, kwa sababu ni sehemu ya kuweka ushirikiano, tuliligusia, unajua Simba inajulikana kila sehemu, hata huku inazungumzwa sana, tukaona tunaweza kufanya haya yanayotokea yasiwe kama wanavyozungumzwa. Tunaamini ni maneno ya kishabiki, nawaomba wachezaji wa Simba wayaache, wao wajikite zaidi uwanjani, akili yao iwe kucheza mpira kwa ajili ya kutafuta ushindi, kwa suala la ulinzi Serikali ya Afrika Kusini haina matatizo," alisema balozi huyo.

Kauli hii ya kuhakikishiwa ulinzi imekuja baada ya kocha wa Orlando Pirates, Mandla Ncikazi, kuzungumza maneno makali, ambayo yameonekana kuwatisha Simba, hivyo kuhitaji ulinzi.

Mbali na hilo, Milanzi alipongeza Simba kwa ushindi waliopata katika mechi ya kwanza wakiwa nyumbani na kusema walicheza vizuri kwa kumiliki mpira kwa kiasi kikubwa, hivyo anaamini wataendelea kufanya vyema.

"Niwapongeze Simba kama kawaida yao, kwa mara nyingine tena wameiwakilisha nchi vizuri, walicheza vizuri sana, na nawaomba katika mechi hii ya marudiano wacheze kama vile, wasicheze kwa kuzuia sana, washambulie pia kwa ajili ya kupata ushindi," Milanzi alisema.

**Naye Barbara alisema wako salama na ana matumaini timu yao itafanya vyema katika mchezo wa kesho.**

"Tumefika, tunajiandaa, tuko vitani na tunashinda Jumapili," alisema Barbara huku akieleza sababu za kutoweka wazi safari yao ya kutua huko Afrika Kusini.

Aliwataka Watanzania wote waliopo Afrika Kusini kwenda uwanjani kuiunga mkono Simba huku waliobaki nyumbani waendelee kuiombea dua njema.

Wakati huo huo, Kocha na mchezaji wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema ili timu hiyo ifanye vizuri katika michuano ya kimataifa msimu ujao, inahitaji kufanya usajili wa wachezaji wapya wasiopungua 10 ili kuimarisha makali yake.

"Ukweli ni kwamba Simba kwa sasa inatakiwa kufanyiwa marekebisho, siyo twende na majina au mazoea. Nafikiri jambo hilo viongozi wanalifahamu, lakini kwa sasa hawawezi kuwaambia watu kuwa tutatoa mchezaji huyu, tutaingiza yule, nani abaki nani atoke, kwa sababu watawavunja nguvu kwani wapo kwenye mashindano. Kimsingi wanawaacha ili waendelee kupambana hadi mwisho wa msimu, na baada ya hapo wapatikene wachezaji watakaokuja kuongeza nguvu," alisema Julio.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >